**6 FEBRUARI, 2026**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA PILI

**Kikao cha Tisa - Tarehe 6 Februari, 2026**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## DUA

Spika *(Mhe. Mussa A. Zungu)* Alisoma Dua

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ENG. MSHAMU A. MUNDE):** Mheshimiwa Spika, kabla ya kuwasilisha Hati Mezani, ninaomba nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai wa kukutana leo hapa tukiendelea na Kikao cha Bunge lako Tukufu. Kwanza nitoe shukrani za dhati kwa wananchi wangu wa Liwale ambao wametupa kura za heshima, mimi na Rais ambaye alipata kura 97%, nami 93%. Kwa maono na kazi alizozifanya ndani ya miaka minne ilisababisha kura hizo za heshima pia na matumaini ambayo tuliwapa kupitia Ilani ya Uchaguzi na sasa wanashuhudia makubwa yanayotekelezwa ndani ya Jimbo letu.

Mheshimiwa Spika, ninakupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote kwa kazi nzuri ambazo mmezifanya na ninawapongeza pia kwa kuchaguliwa.

Mheshimiwa Spika, mjadala ulioendelea hapa wa Kamati ya Bajeti umetupa Wizara ya Fedha uwezo mkubwa wa kwenda kuboresha kupitia maoni na mapendekezo ya Kamati ya Bajeti, Mwenyekiti, Makamu na Wajumbe wote wa Kamati ya Bajeti, ninawapongeza sana kwa kazi kubwa, sina uhakika kama walilala kabla ya kuwasilisha ile taarifa ya Kamati mbele ya Bunge. Ninawapongeza pia Wabunge wote ambao walitoa hoja zao kuanzia Profesa Muhongo mpaka jana Mheshimiwa Nassriya kwa maoni na mapendekezo mazito ambayo wamekuwa wakiyatoa kwenye Kamati ile nasi tutaenda kuzingatia.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo machache ninaomba kuwasilisha Hati Mezani kama ifuatavyo:

Mapitio ya Nusu Mwaka ya Tamko la Sera ya fedha kwa mwaka 2025/2026 *(Monetary Policy Statement Mid-Year Review 2025/2026)*; na

Hati ya Uhamisho wa Bajeti baina ya Mafungu Na.1 kwa Mwaka 2024/2025 *(Statement of Reallocation Between Votes - Reallocation Statement No. 1 of 2024/2025)* na; Hati ya Uhamisho wa Bajeti ndani ya Mafungu Na. 2 kwa Mwaka 2025/2026 kufikia 31 Disemba, 2025 *(Statement of Reallocation Within Votes - Reallocation Statement No. 2 of 2025/2026 as at 31st December, 2025)*.

**SPIKA:** Ahsante.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere. *(Makofi)*

Na. 137

**Ujenzi wa Shule ya Sekondari Sanzate na Tirina – Bunda**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itamaliza ujenzi wa Shule ya Sekondari Sanzate na Tirina - Bunda?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ninaomba uridhie kwamba majibu nitakayoyasoma hapa ndiyo yachukuliwe kama majibu rasmi ya Serikali yale yaliyokuwa tumeyatanguliza yana marekebisho kidogo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali ilitoa Shilingi Milioni 470 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya madarasa manne, jengo la utawala, maktaba, maabara tatu, chumba cha TEHAMA, matundu ya vyoo ishirini na matenki ya kuvuna maji ya mvua, katika shule mpya ya Tirina. Pia, Serikali imetoa Shilingi Milioni 140 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa manne, ofisi moja na matundu nane ya vyoo, ukamilishaji wa madarasa matatu na ofisi moja katika Shule ya Sekondari Sanzate.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2026/2027 Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kukamilisha miundombinu yote iliyobaki kwenye shule hizi mbili za Tirina na Sanzate.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini ninauliza tu maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; TAMISEMI ni lini sasa watakuwa na chombo ambacho kinakuwa kinaangalia kwamba miradi mingi wanayopeleka kwenye maeneo ya vijijini, sekondari na maabara

na vitu vingine, inamalizika na wakae wanajua kwamba imemalizika kikamilifu? Ni lini watakuwa na hicho chombo cha kutazama sekondari ipi haijamalizika wakamalizia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Shule ya Sekondari ya Sanzate imejengwa na wananchi, tumei-*support* milioni 140 yakaja hapa maombi, tumeleta maombi maalum ya milioni 420, ilikuwa bajeti ya mwaka juzi, wakasema itatoka haikutoka, mwaka jana haikutoka. Je, ni lini sasa hizo hela zitatoka ili Shule ya Sanzate imalizike? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye swali langu la msingi mwaka wa fedha 2026/2027 tunakwenda kutenga fedha kwa ajili ya kumalizia miundombinu kwenye shule hizi mbili; Shule ya Sanzate pamoja na Shule ya Tirina. Tunatambua kwamba katika Shule ya Tirina miundombinu ambayo haijakamilika ni maabara tatu, maabara ya *physics, chemistry* na *biology*, vilevile jengo la TEHAMA ambalo hatujakamilisha kuingiza miundombinu ya umeme, tutakwenda kuikamilisha.

Mheshimiwa Spika, kwenye Shule ile ya Tirina tukishatenga fedha mwaka ujao wa fedha tunakwenda kukamilisha kujenga jengo la Utawala, jengo la TEHAMA, maabara tatu pamoja na maktaba ili kuleta ufanisi wa mazingira mazuri ya kujifunzia kwa watoto hawa ambao Mheshimiwa Mbunge Getere amekuwa akiwapambania sana sana na ninamwahidi tutaambatana naye kwenda Jimboni kwa ajili ya kuwatembelea wananchi hawa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na swali la Mheshimiwa Hamoud Juma kwa niaba yake Mheshimiwa Subira.

Na. 138

**Kuupandisha Hadhi Mji Mdogo wa Mlandizi**

**MHE. SUBIRA K. MGALU K.n.y. MHE. HAMOUD A. JUMAA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupandisha hadhi Mji Mdogo wa Mlandizi kuwa Mji kamili?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamoud Abuu Jumaa ambalo leo limewasilishwa na Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu na nimpongeze kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Halmashauri huanzishwa au kupandishwa hadhi kwa mujibu wa Sheria za Serikali za Mitaa, Sura ya 287 na 288 pamoja na mwongozo wa uanzishwaji wa maeneo ya utawala ambao tumeutoa mwaka 2014, ambao umeainisha vigezo na taratibu zinazopaswa kufuatwa ili kuanzisha au kupandisha hadhi Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa mwongozo mchakato wa kuanzisha Halmashauri mpya huanza na kusudio ambalo hupaswa kujadiliwa katika vikao vya ngazi ya Vijiji/Mitaa, Kata, Halmashauri, Wilaya na Mikoa. Kusudio hilo huwasilishwa Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kupitia Katibu Tawala wa Mkoa husika kwa ajili ya kufanyiwa tathmini na ufuatiliaji ili kuhakikisha ufikiwaji wa vigezo husika.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuielekeza Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha kufanya michakato iliyoainishwa kwenye sheria zetu na mwongozo wa uanzishwaji wa maeneo ya utawala.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Subira.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Kwanza ninaishukuru sana Serikali kwa majibu mazuri ya kuleta matumaini.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; kwa kuwa, hii Halmashauri ya Kibaha kwa vigezo imekuwa na vigezo vingi ikiwemo idadi kubwa ya watu imefika 123,000, ikiwemo Serikali kujenga Mji wa Viwanda, maono ya Rais, Kibaha Vijijini, Mji wa Kwala. Je, Serikali ipo tayari yenyewe kuona namna gani ya kuenzi maono ya Mheshimiwa Rais kutokana na Mji wa Kwala na kuupandisha hadhi Halmashauri ya Kibaha Vijijini kuwa Mji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa Serikali yetu imeitangaza Halmashauri ya Bagamoyo kuwa Halmashauri ya Mji na tunashukuru sana hatua mbalimbali zimekamilika na tangazo la Serikali limetoka. Je, ni lini sasa Serikali itaanza mchakato wa kuhakikisha hadhi ya Halmashauri ya Mji wa Bagamoyo kutoka kwenye Vitongoji kwenda kwenye Mitaa na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utafanyika. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Spika, sheria yetu pamoja na Mwongozo wa Uanzishwaji wa Mamlaka za Kiutawala wa Mwaka 2014 umeweka vigezo vingi lakini vigezo vikubwa ni vitatu.

Mheshimiwa Spika, kigezo cha kwanza ni kigezo cha uwezo wa kujiendesha kwa kutumia mapato ya ndani, hapa tumeweka uwiano Halmashauri Mama inapotenganishwa na kuanzisha Halmashauri mpya ya Mji, ile Halmashauri mpya ya Mji inatakiwa iwe na uwezo wa kujiendesha kwa mapato ya ndani kwa 30% na ile Halmashauri mama inayobaki inatakiwa iwe na uwezo wa kujiendesha kwa kutumia mapato ya ndani kwa 20% na hivyo kufanya hitajio la kujitegemea kwa 50%.

Mheshimiwa Spika, kigezo cha pili ambacho ni kikubwa na kimewekwa ni kigezo cha idadi ya watu na hii ni kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi, lipo hitajio kwamba Halmashauri mpya inayoanzishwa kwa maana ya Halmashauri ya Mji iwe na idadi ya watu wasiopungua 150,000 na ile inayobaki kwa maana ya Halmashauri mama inatakiwa iwe na watu 250,000.

Mheshimiwa Spika, lipo hitajio la tatu ambalo ni la muhimu zaidi katika yale mengi yaliyopo, ni angalau kwenye ile Halmashauri ya Mji tunayoanzisha iwe na watu 30% wanaojishughulisha na shughuli ambazo siyo za kilimo. Kwa hiyo, nirudie tena kuwaelekeza Halmashauri ya Kibaha wapitie vigezo hivi, wapitie sheria zetu na kama wanakidhi vigezo hivi waendelee na mchakato huo nasi TAMISEMI tutakuwa tunasubiria kwa ajili ya kutekeleza wajibu wetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bagamoyo ni kweli tumeitangaza kwa maana ya kuwa *gazetted* Bagamoyo kuwa Halmashauri na sisi ndani ya Serikali mchakato haujasimama kama ambavyo tumeendelea tumetangaza, sasa tunaendelea na mambo ya kibajeti na mipango ya nchi yetu ili tuweze kuendelea kwenye hatua iliyobaki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ado.

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona ili niulize swali dogo la nyongeza. Mbunge wa Tunduru Kusini Mhandisi Fadhili Chilombe, ninafahamu kwamba ameleta hoja na kufuatilia mara nyingi Wizara ya TAMISEMI juu ya haja ya kuigawanya Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru kupata Halmashauri mbili na mchakato wetu ulifika mpaka *RCC,* tuna watu zaidi 400,000 na tuna kilometa za mraba 18,000.

Mheshimiwa Spika, tunataka kauli ya TAMISEMI ili Watanzania wanaoishi Tunduru wapate kauli ya Serikali ndani ya Bunge. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kujibu kwenye jibu la msingi, uanzishwaji wa mamlaka za kiutawala ikiwemo hili analoliongelea Mheshimiwa Mbunge, Ado Shaibu, Mwenyekiti wetu wa Kamati ya *LAAC* unazingatia Sheria ile ya Uanzishwaji ya Mamlaka za Wilaya, Sura Na. 287 pamoja na Sheria ya Uanzishwaji wa Mamlaka za Miji, Sura 288.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimetoa maelekezo na ushauri kwa Halmashauri ya Kibaha, vivyo hivyo wananchi wa Tunduru wafuate utaratibu huo na TAMISEMI kazi yetu ni moja tu kufanya tathmini na mapitio kama vigezo vimezingatiwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Patali.

**MHE. PATALI S. PATALI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii nami nipate kuuliza swali la nyongeza kutoka kwenye swali la msingi Na. 138. Je, ni lini Serikali itaupandisha hadhi Mji Mdogo wa Mbalizi kuwa Mamlaka ya Mji kamili, ikizingatiwa mji huu umekidhi vigezo vyote ikiwepo idadi ya watu, uwezo wa kujiendesha wenyewe? Pia mji huu umeomba kupandishwa hadhi muda mrefu sana?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kwa niaba ya Wanambeya Vijijini nipate majibu ya Serikali. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Spika, ninawaelekeza uongozi wa Mkoa, husika wakamilishe michakato yote ambayo imeainishwa kisheria, ikiwa ni pamoja na kuanza mijadala kwenye ngazi ya Mitaa na Kata, Wilaya kwenye vikao vya *RCC,* vikao vya *DCC*. Watakapokamilisha wawasilishe TAMISEMI kama utaratibu unavyotaka, TAMISEMI tutatuma timu na tutafanya mapitio ya vigezo hivyo na kama vigezo vitakidhi, mamlaka itachukua hatua zinazofuata. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Dkt. Yahya Esmail Nawanda.

Na. 139

**Ujenzi wa Barabara za Jimbo la Newala Vijijini**

**MHE. DKT. YAHYA E. NAWANDA** aliuliza:-

Je, lini Barabara za Chikalule hadi Lihanga na Lochinu hadi Mkwiti zitajengwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Yahya Esmail Nawanda, Mbunge wa Newala Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutenga bajeti na kujenga barabara katika miinuko mikali kulingana na upatikanaji wa fedha ambapo hadi sasa imeshajenga Barabara ya Miyuyu hadi Hospitali ya Rufaa ya Ndanda yenye urefu wa kilometa 4.5 kwa tabaka la lami kwa gharama ya shilingi bilioni 2.25. Aidha, ujenzi wa kilometa 0.6 kwa kiwango cha zege kwenye eneo la mwinuko mkali katika Barabara ya Namdimba - Chiwata kwa gharama ya Shilingi Milioni 975.98 unaendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na ujenzi wa barabara ambazo zipo kwenye maeneo ya milima mikali katika Jimbo la Newala Vijijini, zikiwemo Barabara za Lihanga na Chikalule kilometa 1.5 na Barabara ya Mkwiti - Lochino - Nyangao kilometa 11.1 kulingana na upatikanaji wa fedha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Nape.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru na ninaomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Barabara hii ya Mkwiti ni barabara ambayo inatuunganisha Mtama na Newala Vijijini na

Newala Mjini na ni barabara ya uchumi mkubwa kwa sababu uchumi mkubwa wa korosho unatokea…

**SPIKA:** Mheshimiwa samahani, Mheshimiwa Nawanda anaanza mwenye swali la msingi.

**MHE. DKT. YAHYA E. NAWANDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; Mfuko wa Barabara umekuwa unagharamia zile barabara ambazo ziko rasmi na umekuwa unajenga Barabara kutoka Mkoma Sokoni hadi Lihanga. Je, ni lini sasa Serikali itatenga fedha maalum kwa ajili ya kumalizia sasa kutoka Lihanga mpaka Chikalule, ambayo ni kama kilometa moja?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa Barabara ya Mchemo hadi Mahuta imekuwa ina changamoto kubwa sana. Je, ni lini Serikali sasa itapandisha hadhi ya barabara hii kutoka udongo kwenda kutengenezwa kuwa barabara changarawe ili wananchi wa maeneo haya waweze kupita kwa usalama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Spika, ninatambua kuwa jiografia ya Mji wa Newala Vijijini ina miinuko mikali na barabara hii ambayo imetajwa na Mheshimiwa Mbunge, Barabara ya Chikalule kwenda Makao Makuu ya Kitangali wananchi wetu kwenye maeneo yale wakati mwingine wamelazimika kupitia Lindi ili kufika makao makuu ya wilaya. Kwa kutambua umuhimu huo pia zipo taasisi kwenye eneo hilo, ikiwemo Shule yetu ya Msingi Chikalule ambayo inafanya vizuri sana; na ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa niaba ya wananchi wale.

Mheshimiwa Spika, Serikali itakwenda kuijenga barabara hii kwa kadri ya upatikanaji wa fedha. Tumepanga, kwenye Mwaka wa Fedha unaofuata wa 2026/2027 tutaweka fedha kwa ajili ya barabara hii.

Mheshimiwa Spika, siyo hivyo tu, kwenye swali lake la pili ameitaja Barabara ya Mchemu hadi Mahuta na Mheshimiwa Nape wakati ameanza kuuliza alitaka kuitaja barabara hii. Tunatambua kuwa barabara hii imebeba uchumi mkubwa wa zao la korosho kwenye maeneo ya Newala pamoja na Tandahimba na ina urefu wa kilometa 17.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha ujao ninawaelekeza mkoa waiangalie barabara hii vizuri ili waihuishe kwenye mipango yetu ya kitaifa na hatimaye iweze kujengwa na kuinua uchumi na kufungua uchumi wa Wananewala pamoja na Wanatandaimba.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nape.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Hoja yangu ya msingi ilikuwa ni kwamba hii Barabara ya kutoka Mtama kwenda Newala Vijijini hadi Newala Mjini kama nilivyosema ni barabara kubwa ya uchumi mkubwa na inaunganisha mikoa miwili, Mtwara na Lindi na wilaya zetu. Barabara hii imekuwa ikijengwa kidogo kidogo sana, yaani fedha inatoka kidogo kidogo sana. Ni wakati sasa Serikali iamue kutoa fedha kuimaliza badala ya kuwa inajenga hivi kidogo kidogo na uchumi wetu unaendelea kudorora kwenye eneo hili husika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Spika, tunatambua umuhimu wa barabara hii. Kama nilivyotangulia kusema, barabara hizi tutazitengea fedha kwenye mipango yetu. Kwenye eneo hili si barabara hiyo tu yenye umuhimu, ipo Barabara ya kutoka Maputi kwenda Ndanda, pia iko Barabara ya kutoka Chiwonga, Pacha Nne hadi Nanganga njia panda ya kwenda Ruangwa. Zote hizi ni barabara tunazozitazama kwa jicho la ukaribu na tutakwenda kuhakikisha kwamba barabara hizi zinafunguka. Ni dhamira ya Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwamba uchumi unafunguliwa, barabara zinafunguliwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kaegele.

**MHE. MOSES L. KAEGELE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. Kijiji cha Tundu ni kijiji chenye wakazi zaidi ya 3000 na kijiji hicho kipo pembezoni mwa Ziwa Tanganyika, namna pekee ya kufikia pale kijijini ni njia ya maji. Tokea ziwa limechafuka wakazi wa pale hawafikiki. Je, ni lini serikali itatenga fedha kwa ajili ya kufungua Barabara kutoka Kala kwenda Tundu na kujenga madaraja mawili ili wananchi hawa waweze kupata huduma za msingi kwa wakati?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Spika, ninaomba nikiri kuwa Mheshimiwa Mbunge alikwishakuja ofisini kwenye ofisi zetu za TAMISEMI. Tumekwishakaa na watalam, tumeangalia umuhimu wa barabara hii ambayo ipo pembezoni kabisa, lakini inaenda kwenye kata yenye wakazi zaidi ya 3000. Kupitia mradi wetu wa Mheshimiwa *RISE* tunaangalia uwezekano wa kuweka madaraja; ambapo yanahitajika madaraja takribani matatu; ili tuweze kufungua uchumi kwa eneo lile na kusaidia wananchi wetu wa eneo lile.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Neema Peter Majule.

Na. 140

**Mfumo wa Kupima Matokeo ya Mikopo ya Asilimia 10**

**MHE. DKT. NEEMA P. MAJULE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Mfumo madhubuti wa kupima matokeo ya mikopo 10% ya Halmashauri ili kubaini changamoto na mafanikio?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Dkt. Neema Peter Majule, Mbunge wa Mkoa mzima wa Dodoma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kanuni za 31, 32 na 36 za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu za Mwaka 2024 zinaelekeza na kuweka utaratibu wa kufanyika kwa tathmini ya utoaji na usimamizi wa mikopo kila mwaka katika ngazi ya Halmashauri Mkoa na Taifa. Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI imekwishafanya tathmini mara moja tangu kuanza kwa mfumo mpya wa utoaji mikopo. Pia tathmini imekuwa ikifanyika kulingana na changamoto ambazo zinajitokeza wakati wa utekelezaji. Tathmini hizi ndizo zinazowezesha kufanya maboresho mbalimbali mifumo inayotumika.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Januari, 2026, jumla ya vikundi 24,064 vimepata mikopo, ambapo vikundi vya wanawake ni 13,639, vijana ni 8,140 na watu wenye ulemavu ni 2,285. Serikali pia imejenga uwezo kwa wasimamizi 736 wa Halmashauri na 78 wa Mikoa kuhusu usimamizi wa Mfumo wa WEZESHA na inaendelea kuufanyia maboresho Mfumo wa Wezesha ili kuongeza ufanisi na tija ya mikopo kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Neema.

**MHE. DKT. NEEMA P. MAJULE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ya kwamba tathmini ilifanyika na bado kuna maboresho yamefanyika, lakini bado kumekuwa na malalamiko makubwa kwa wanawake wa Dodoma Vijijini kwamba mikopo hii haiwafikii na pia kumekuwa na mchakato mrefu sana wa upatikanaji wa mikopo hiyo. Je, ni lini Serikali itakuwa na njia mbadala kwa ajili

ya wanawake wa vijijini kupata mikopo sawa na wanawake wa mijini ambao wapo karibu na hizo fursa?

Mheshimiwa Spika, lingine pia kumekuwa na huo mchakato mrefu...

**SPIKA:** Mheshimiwa hujauliza maswali mawili?

**MHE. DKT. NEEMA P. MAJULE:** Mheshimiwa Spika, hili ni swali la pili la nyongeza.

**SPIKA:** Sawa, endelea.

**MHE. DKT. NEEMA P. MAJULE:** Mheshimiwa Spika, kumekuwa na mchakato mrefu wa upatikanaji wa huduma hii ya mikopo, kwamba, wanawake wengine wamekata tamaa kabla hawajafikia kupata mikopo. Swali, je, ni lini Serikali itakuja sasa na *one stop centre* ambapo mwanamke huyu akienda atakuta na atapata pale pale katiba, cheti, *tax clearance*, *service levy* na huo mkopo ili kunusuru wanawake kukata tamaa ku-*process* mkopo huu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Spika, ninaomba niyajibu maswali yote mawili kwa pamoja kwa sababu yanaingiliana.

Mheshimiwa Spika, wote tutakumbuka kwamba mara baada ya kuanzisha utoaji wa mikopo awamu mpya, kwa maana ya baada ya kuachana na utaratibu wa zamani, Serikali ilizigawa halmashauri zetu katika makundi mawili. Kundi la kwanza likiwa na halmashauri 174 na kundi la pili, ikiwemo Dodoma, likiwa na halmashauri 10. Halmashauri 174 tumeendelea kutoa mikopo kupitia utaratibu ulioboreshwa, lakini halmashauri hizi 10 pia tulisema tutoe mikopo kupitia benki ili tuweze kuona kama tutafanikiwa, kama ambavyo Mheshimiwa Rais alikuwa ametamani ifanyike, hatimaye tuweze kufanya utaratibu wote utumike kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, sasa katika mikoa 10, maeneo 10 ambayo tulipanga kufanya kupitia benki ni pamoja na Jiji la Dar es Salaam, kwa maana ya Mkoa mzima wa Dar es Salaam, Dodoma, Songea Manispaa, Newala, Bumbuli, Siha, Mbulu pamoja na Itilima na Nkasi; huku kote tumeendelea kutoa kupitia utaratibu wa benki.

Mheshimiwa Spika, wiki mbili zilizopita tumekaa na benki hizi tatu ambazo tulikuwa tumezipa kazi hii; Benki za *CRDB, NMB* na *Uchumi Commercial Bank;* kwa ajili ya kufanya tathmini na kuona maeneo ambayo yamekuwa kikwazo kwa watu wetu.

Mheshimiwa Spika, msisitizo wetu na namna ambayo tumekubaliana na maelekezo ambayo tumepeana ni kwamba, mabenki ni sharti yazingatie kwamba wananchi ambao tunataka wakopeshwe mikopo hii, ni wananchi ambao hawawezi kukidhi masharti ya kibenki. Ndiyo maana tumesaini *MoU* ya kuhakikisha kuwa wanapewa kwa mazingira hayo hayo waliyonayo. Mheshimiwa Rais anataka watu wote wapate mikopo, hata wasiokopesheka kwenye benki. Kwa hiyo nisisitize tena kwamba tutayasimamia haya ili kuhakikisha hakuna ucheleweshwaji wa utoaji wa mikopo.

Mheshimiwa Spika, jana tumejibu swali hapa na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI amelitolea maelezo marefu na ya kina, kwamba Maafisa Maendeleo ya Jamii kwa kushirikiana na TAMISEMI wamewezeshwa. Kwanza pikipiki zaidi ya 98 ili waweze kuwafikia wananchi wetu kwenye vikundi vyao mahali walipo; na pia Serikali kupitia TAMISEMI tumekuwa tukitenga fedha kwenye *OC* zetu. Kila tunapopeleka *OC* tunapeleka na fungu kwa ajili ya Mafisa Maendeleo ya Jamii kuweza kuwafikia watu wetu. Niwaelekeze mikoa yote kupitia ma-*RAS* wetu wahakikishe kuwa hapawi na usumbufu wote kwa wananchi kupatiwa mikopo hii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, shida Serikali imefanya vizuri sana, watendaji wako wamefanya kazi vizuri sana, ma-*DC* wamefanya vizuri sana, kata zimefanya vizuri sana; shida ni benki hawatoi fedha. Kwa hiyo kwa upande wa Serikali tunawapongeza kwa kuwa mmetimiza azma ya Mheshimiwa Rais. Fedha hizi si sadaka, fedha hizi si za bure, zikopo hizi zirudi

zizunguke. Wananchi wamekubali, tatizo benki haziwafikii, masharti yao magumu. Kwa hiyo kama hii ni *pilot project*, mjue kabisa kwa hii *project* mkiwatumia benki ambao hawana urafiki na watu kwa kipato cha chini hili zoezi litakuharibia heshima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Shingo, Mheshimiwa Shingo, ulisimama.

**MHE. BAKARI B. SHINGO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na nina swali dogo la nyongeza. Katika Jimbo langu la Ukonga, hasa Halmashauri yetu Jiji la Dar es Salaam moja ya mambo yaliyopelekea halmashauri ikahamisha utaratibu wa kukopesha moja kwa moja ni baadhi ya watumishi wa halmashauri na baadhi ya Madiwani walisemwa kwamba wamekuwa wakitumia mlango wa nyuma kujikopesha, lakini pia kuwepo na vikundi ambavyo sasa vimekopeshwa zaidi ya mamilioni na vimetajwa kuwa havionekani.

Mheshimiwa Spika, swali langu ni kuwa; je, kwa ajili ya kulinda maslahi mapana ya Taifa na kodi zetu, ni kwa nini Serikali isiweke utaratibu wa kuyataja hadharani hayo makundi ama hivyo vikundi vilivyokopa ambavyo sasa havionekani, sambamba na baadhi ya watumishi wa halmashauri ambao siyo waaminifu waolijingiza katika mtego huu ambao leo unapelekea halmashauri zetu kuhamisha Mfuko huo kupeleka kwenye benki, benki ambazo zinasababisha tushindwe kupata mikopo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi. Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, nilikuona.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ambayo Naibu wangu ameyatoa, kama alivyosema, tulikuwa na kikao na benki hizi. Kilichotokea ni kwamba, kweli kwenye majiji kuna fedha nyingi ambazo hazijakopeshwa uki-*compare* na kwenye halmashauri za wilaya na miji. Shida iliyopo, kutokana na maelezo waliyotupa benki; la kwanza, ni kweli kwamba walikuwa na masharti magumu, lakini kwa sasa sharti linalotakiwa kwa mtu kwa kikundi kukopa ni wale wanakikundi kuwa na *NIDA*.

Mheshimiwa Spika, nini kimesababisha sasa majiji yawe na fedha nyingi; wamesema, ni kwa sababu wale wanaounda vikundi walioko Dar es Salaam kwa mfano wanakutana kimjini mjini, kwa hiyo hawawezi na inakuwa ngumu sana kupata kikundi kimoja cha watu ambao wanaweza kukopeshwa kwa wakati huo. Hii ni kwa sababu, huyu ametoka Segerea, mwingine ametoka Ubungo, mwingine tena ametoka Kawe na wanakutana Kariakoo kwenye biashara. Wakiwa pale kila mtu hajui huyo mwenzake ametokea wapi.

Mheshimiwa Spika, *proposal* ya benki ni kwamba, ikiwezekana tuwape mikopo *individuals* kama tunavyofanya kwa walemavu; lakini tuwe na *condition* moja kwamba huyu *individual* tunayempa mkopo atuhakikishie kwamba kwanza ana biashara, ana leseni ya biashara; lakini pili, ataweza ku-*employ* angalau watu watatu kwenye ile biashara kutokana na mkopo tunaowapa.

Mheshimiwa Spika, kama hii itafanyika, kitu cha kwanza zile bilioni zilizolala kule benki zitatoka. Kitu cha pili, tutaona kwamba tume-*create* ajira kwa vijana ambao ni moja ya vitu ambavyo tunaviangalia sana kwenye fedha hii. Kwa hiyo Bunge lako hili ninaomba lielewe kwamba, tutakwenda kuona namna ya kubadilisha ule mwongozo na kukubali kwamba tuwe na *pilot* ya majiji ya kutoa mikopo kwa *individuals* ambao watatuhakikishia kwamba wata-*create* ajira kwenye maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, nimeomba nisimame nitoe ufafanuzi huu na kushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ninakushukuru sana; lakini sisi wote ni Waheshimiwa Wabunge; nitakupa mfano kuna Kikundi kinaitwa *Two in One* kipo kariakoo, wote wakazi wa Kariakoo; huu mwaka wa pili wanazungushwa, wamekamilisha kila kitu; na hicho kikundi kimoja tu. Kwa hiyo benki nao walete uthibitisho. Nina uhakika kwamba benki hawana *capacity* ya kufikia vikundi vyote hivi, hawana.

Serikali imefanya kazi nzuri sana, vikundi vyote vimekaguliwa na watendaji, vyote; lakini vikishafika benki wanataka leseni ya *fire, TIN number.* Sasa mamalishe, bibi yetu pale, Bi Shukuru *TIN number* anaitoa wapi? Leseni ya *fire* anaitoa wapi? Tujali maisha ya watu. Hawa watu wetu kipato chao cha chini.

Mheshimiwa Waziri mkikaa na *degree* za uchumi hatutoweza kuwasaidia hawa wananchi. Wananchi washirikishwe, waambiwe kuwa fedha hizo si sadaka na kwamba fedha hizo ni za mkopo. Kopa milioni rudisha milioni bila riba. Kwa hiyo ninakuomba sana. Tena hawa watu wa benki waite tuje kuwaona. Tuje kukaa na Waheshimiwa Wabunge hapa, sawa? Ahsante.

Mheshimiwa Dkt. Majule ninafikiri swali lake limekwishajibiwa. Mheshimiwa Zuberi Yahya Mfaume.

Na. 141

**Kudhibiti Migogoro ya Wakulima na Wafugaji – Morogoro Kusini**

**MHE. ZUBERI Y. MFAUME** aliuliza:-

Je, lini Serikali itadhibiti migogoro ya wakulima na wafugaji katika maeneo ya Mvuha, Selembala, Dutumi, Kisaki, Bwakila Juu, na Kolelo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Zuberi Yahya Mfaume, Mbunge wa Morogoro Kusini:-

Mheshimiwa Spika, kipindi cha kiangazi hutokea adha ya upungufu wa malisho maeneo mengi, ambapo hupelekea wafugaji kuanza kuhama kwa ajili ya kutafuta maji na malisho. Hali hii inasababisha wimbi la wafugaji vamizi kutoka nje ya Wilaya

ya Morogoro kuleta mifugo mingi ambayo husababisha mwingiliano na uharibifu wa mazao.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na migogoro, ikiwa ni pamoja na kutenga na kutambua maeneo ya malisho kwa wafugaji kupitia mpango wa matumizi bora ya ardhi, ambapo jumla ya vijiji 68 vimefanyiwa mpango wa matumizi ya ardhi kwa kutenga hekta 54,577. Watendaji wote wa vijiji na kata kutoruhusu wafugaji wageni kuingia kwenye maeneo yao bila kufuata taratibu, kuhamasisha uzalishaji wa malisho ili kuongeza upatikanaji wa malisho kwa wafugaji.

Mheshimiwa Spika, wizara za kisekta zimeendelea kuimarisha huduma za ugani kwa kutoa elimu ya ufugaji wenye tija wa kuwa na mifugo michache.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na vyombo vingine ya ulinzi na usalama kufanya operesheni maalum ya kuondoa mifugo kwenye maeneo ya mashamba ya wakulima katika Wilaya ya Morogoro. Pia, Serikali inapopata tetesi ya mgogoro kwa wafugaji na wakulima, Viongozi ngazi ya Mkoa na Wilaya hufika kwa wakati na kuhakikisha migogoro inatatuliwa.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Zuberi.

**MHE. ZUBERI Y. MFAUME:** Mheshimiwa Spika, ninaomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza kutokea katika swali langu la msingi.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; mpaka hivi sasa ninavyozungumza hapa bado kuna mifugo katika mashamba ya wakulima huko katika Jimbo la Morogoro Kusini. Nini kauli ya Mheshimiwa Naibu Waziri sasa hivi ili iweze kutekelezwa na mifugo hiyo iondolewe katika mashamba ya wakulima?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Wizara ina mpango gani sasa katika Jimbo la Morogoro Kusini kuongeza ujenzi wa majosho, malambo pamoja na kasi ya kuelimisha wafugaji juu ya ufugaji bora wa kisasa? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali mawili madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Mfaume, Mbunge wa Morogoro Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze kwa maswali yanayogusa changamoto hizi za wakulima na wafugaji. Sisi Ofisi ya TAMISEMI tunashirikiana kwa karibu sana na Wizara ya Uvuvi na Mifugo na wameendelea kutoa elimu wenzetu Wizara ya Mifugo na pia wanatoa mbegu za ruzuku kwa ajili ya malisho ili kuondoa migogoro hii kabisa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, tunaendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya ulinzi na usalama kuhakikisha mifugo inaondolewa katika maeneo ya wakulima wetu na baadae nitakaa na Mheshimiwa Mbunge pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Mifugo ili tuweze kuyaangazia maeneo haya na kupata ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali imeendelea kujenga majosho mengi nchini. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge tuweze kuainisha eneo ambalo hasa amelizungumzia ambalo halijapata majosho mpaka sasa ili tuweze kujenga majosho hayo.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Lucy Kombani.

**MHE. LUCY D. S. KOMBANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa hii migogoro imekuwa ya muda mrefu sana na inaleta madhara makubwa sana kwenye hizi jamii zetu na kwa upande mwingine tukiangalia tuna wataalam ambao wamesomea utatuzi wa migogoro; je, Serikali haioni haja sasa ya kuwatumia wataalam hawa katika kumaliza haya matatizo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwa kipindi cha mwaka 2023 hadi 2025 hakujaripotiwa migogoro yenye kuleta mapigano katika maeneo mengi nchini. Serikali inamuahidi Mheshimiwa Mbunge tutaendelea kuwatumia wataalam hawa ili kuweka hali hii ya usalama wa wakulima na wafugaji. Tunaendelea kuhamasisha zile kampeni (kwa mfano, Kampeni ya Tutunzane) ili kuona kabisa wakulima na wafugaji wanavyohitajiana na waweze kuishi katika maeneo kwa usalama na uzalishaji mali uendelee.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhata.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Spika, ndani ya Jimbo langu la Nanyumbu hivi ninavyozungumza kuna mgogoro mkubwa wa wafugaji na wakulima na kusababisha mashamba ya wakulima kuliwa na mifugo ya wafugaji. Je, Serikali ina kauli gani kuwalazimisha hao wafugaji ambao wamesababisha hasara kubwa kwa wakulima waweze kulipa gharama zote za uzalishaji na badala yake kuwaachia Polisi kushughulikia suala hilo? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mhata, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia migogoro ya wakulima na wafugaji ni eneo *sensitive* sana na Serikali huwa haijiweki katika eneo la kupendelea, hivyo niwaelekeze wahusika wote wa halmashauri za vijiji na halmashauri zetu waweze kufuatilia mgogoro huo na waripoti kwa wakati ili tuweze kwenda kutatua tatizo hilo. Hata hivyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge

tunaweza kuonana baadaye ili tuweze kuona namna gani ya kuli-*handle* hili bila kuleta *pressure* katika pande zote. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Mattar.

Na.142

**Fedha za Mazingira Zanzibar**

**MHE. MATTAR ALI SALUM** aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kuongeza wigo wa fedha za mazingira ili kusaidia juhudi za Zanzibar kukabiliana na athari hizo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mattar Ali Salum, Mbunge wa Jimbo la Shaurimoyo kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuhakikisha zinaongeza wigo wa fedha za mazingira kupitia vyanzo vya mapato ya ndani na nje ili kusaidia juhudi za Zanzibar kukabiliana na athari hizo.

Mheshimiwa Spika, hatua hizo ni pamoja na: kutenga fedha kupitia Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kutafuta fedha kutoka katika Mifuko mbalimbali ya Kimataifa ya Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi ambayo ni pamoja na Mfuko wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi *(Adaptation Fund),* Mfuko wa Mazingira wa Dunia *(Global Environment Facility)* na Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi *(Green Climate Fund)* na kuendelea kushirikiana na Wadau mbalimbali wa Maendeleo ili kuongeza wigo wa fedha katika eneo la mazingira.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zitaendelea kuongeza fedha za Mazingira kadri ya fedha za miradi zitakavyokuwa zinapatikana. Hadi sasa, jumla ya miradi 10 yenye thamani ya takribani shilingi bilioni 97.6 imetekelezwa na kukamilika kwa pande zote mbili za Muungano. Aidha, Serikali ipo katika maandalizi ya miradi mitatu yenye thamani ya takribani shilingi bilioni 62.6 ambayo ipo kwenye hatua za awali za maandalizi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mattar.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini kwanza nichukue fursa ya kumpongeza sana Mheshimiwa *Engineer* Masauni kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Baraza la Mazingira la Umoja wa Mataifa. Hili ni jambo jema kwa nchi yetu na ni fursa kwa nchi yetu, lakini Mheshimiwa Waziri Serikali yetu itafaidika vipi na fursa za kifedha katika taasisi hiyo? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Mattar Ali Salumu, Mbunge wa Shaurimoyo kwa kuwa mdau mzuri wa mazingira na kwa kuwasemea wananchi wa Jimbo la Shaurimoyo Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zinao mkakati mahususi wa kuongeza fedha za mazingira kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunahifadhi na kutunza mazingira yetu kwa sababu tunafahamu mazingira ni uhai na hivi sasa katika Mpango wa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025/2050 suala la mazingira limepewa nguzo mahususi na Serikali ya Zanzibar pamoja na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Tutaendelea kuhakikisha kwamba tunaongeza vyanzo na kutunza mazingira. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Kwa kuwa ni miaka mitatu sasa taarifa ya Wizara ya Mazingira na Wizara zingine mtambuka kuhusu Maziwa ya Babati, Basutu, Tlawi kule Mbulu na Mkoa wa Manyara kwa ujumla haijarudishwa na kazi haijafanyika; je, ni lini Waziri atakwenda Mbulu kutembelea hayo Maziwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri mhusika. Mheshimiwa Dokta, Waziri amesimama.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi hii. Ninaomba kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ya maswali yote mawili ya Waheshimiwa Wabunge. Vilevile, nimshukuru Mheshimiwa Mattar na Mheshimiwa Spika wewe pia, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunipongeza jana na leo kwa kuweza kuchaguliwa kwenye nafasi ya Makamu wa Rais wa Baraza la Mazingira la Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba niongezee sasa kujibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni dhahiri kabisa nafasi hii ambayo tumeipata inachangiwa na kazi kubwa na mafanikio makubwa na heshima kubwa ambayo Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan na nchi yetu iliyojenga katika Jumuiya ya Kimataifa ndiyo ikawezesha kuweza kupata heshima hii ya kuweza kupata nafasi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kupitia nafasi hiyo tunaweza kunufaika katika masuala mengi; moja ni kuhakikisha kwamba tunapenyeza vipaumbele vyetu kama Taifa katika kukabiliana na changamoto za mazingira ikiwemo mabadiliko ya tabianchi, upotevu wa Bioanuwai, masuala mengine mbalimbali yanayohusu ikiwemo

nishati safi na kadhalika. Hiyo pia itatusaidia kuweza kunufaika na fedha mbalimbali (fursa za kifedha) kupitia Mifuko ya Mazingira kwenye Jumuiya ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge wa Mbulu aliuliza swali la Ziwa Babati. Ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba yeye pamoja na Mheshimiwa Mbunge wa Babati Mjini tulizungumza nao kuhusiana na jambo hilo. Hivi sasa ninavyozungumza leo kuna timu ya wataalam imekwenda kule Babati kufanya tathmini ili kuhakikisha kwamba tunafanya nini kwa kupata hatua za dharura za kuweza kukabiliana na tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo, Serikali ina mkakati wa muda mrefu ikiwemo kununua mitambo ya kukabiliana na changamoto ya magugu maji katika maeneo yote yaliyoathirika na magugu maji katika nchi yetu. Kwa hiyo, hatua za kwanza za dharura tayari tumeanza nazo leo, lakini baada ya muda siyo mrefu tayari tutapata fedha kupitia Serikali Kuu (kupitia Hazina) ili tuweze kupata mitambo ya kukabiliana na tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante. Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia, Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga.

Na. 143

**Changamoto ya Mawasiliano - Tabora Mjini**

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA** aliuliza:-

Je, lini changamoto ya Mawasiliano Jimbo la Tabora Mjini Kata za Ikomwa, Ndevelwa, Ntalikwa, Kabila, Kalunde na Itetemia itamalizika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mbunge wa Jimbo la Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa kupitia *UCSAF* na watoa huduma wa Mawasiliano ilifikisha huduma za mawasiliano katika Kata husika kama ifuatavyo: Kata ya Ikomwa *(Airtel, Vodacom na Halotel)*, Kata ya Ndevelwa *(Halotel)*, Kata ya Ntalikwa *(Airtel)*, Kata ya Kabila *(Honora, Airtel* na *Halotel)*, Kata ya Kalunde *(Honora, Vodacom, Airtel* na *Halotel)* na Kata ya Itetemia *(Halotel)*.

Mheshimiwa Spika, Kata zote sita zimefikiwa na watoa huduma za mawasiliano kama nilivyotangulia kuwataja kwa kuzijengea minara ambayo imekamilika na inafanya kazi. Kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge ameuliza swali lake kwa kuonyesha kuna tatizo la Mawasiliano, Wizara kwa kushirikiana na *UCSAF* na Watoa Huduma wa Mawasiliano itatuma wataalam katika Jimbo la Tabora Mjini ili kufanya tathmini ya kina ya hali ya mawasiliano kwa lengo la kujua tatizo lililopo.

Mheshimiwa Spika, upo uwezekano wa kutokea tatizo la kupatikana kwa mawasiliano ya uhakika katika baadhi ya maeneo hata kama minara ya mawasiliano ilishajengwa katika maeneo hayo kwa sababu kama vile ongezeko la watu, kukua kwa shughuli za kiuchumi pamoja na jiografia ya eneo husika. Pia, sababu nyingine ni kuanzishwa kwa makazi mapya katika maeneo ambayo awali hayakuwa na wakazi, hivyo kuongeza uhitaji wa kujengwa minara zaidi au kuboreshwa kwa minara iliyopo.

Mheshimiwa Spika, tathmini itakayofanyika itatoa suluhisho sahihi, kama ni kuongeza nguvu ya mitambo katika minara iliyopo au kujenga minara mipya. Iwapo suluhisho ni ujenzi wa minara mipya, Kata husika zitajumuishwa katika miradi itakayotekelezwa kwa kadri ya upatikanaji wa fedha. Aidha, kupitia Mradi wa

Awamu ya 11 utakaotangazwa mwishoni mwa mwezi Februari, Kata ya Ndevelwa, Kijiji cha Itulu utajengwa mnara wa mawasiliano.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; bado Jimbo la Tabora Mjini kwenye kata za pembezoni nilizozitaja hapo zina changamoto kubwa sana ya mawasiliano. Kuna baadhi ya maeneo walitoa maelekezo ikajengwe minara hiyo ya *Halotel* lakini haijajengwa. Nini mpango wa Serikali kwenda kujenga hata hiyo Minara ya *Halotel* wanayoisema ili wananchi wa kata hizi za pembezoni zilizoko kwenye Jimbo la Tabora Mjini waweze kupata mawasiliano ya uhakika?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; pamoja na sasa hivi kuwa tuko kwenye awamu ya uwezo wa mitandao yetu *5G* lakini mpaka leo Tabora Mjini bado tunapokea mawasiliano kwa kutumia *2G*. Nini mpango na mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba wanapeleka minara yenye nguvu ya uwezo wa kupeleka *5G* ili wananchi wa Jimbo la Tabora Mjini ambalo linakua kwa kasi waweze kupata mawasiliano ya uhakika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Hawa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa minara kwenye maeneo aliyoyataja pembezoni mwa Mji wa Tabora, kama nilivyoeleza kwenye jibu la swali namba 74 nilieleza kwamba tunatambua changamoto ya mawasiliano katika maeneo mbalimbali nchini na tuna mkakati mahususi wa miaka mitano kuanzia mwaka huu 2025 mpaka 2030 ambapo tutayafikia

maeneo yote yenye changamoto za mawasiliano ikiwemo ni pamoja na eneo lake la Tabora Mjini.

Mheshimiwa Spika, kwenye maeneo ambayo yana minara na ambayo bado yana changamoto ya mawasiliano, tutatuma wataalam wetu wakafanye tathmini na pale ambapo kutaonekana kuna uhitaji wa kuiongezea nguvu hiyo minara tutaiongezea nguvu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu changamoto ya kuwepo minara ya *2G* katika maeneo ya mjini. Ni kweli bado kuna maeneo hapa nchini yanasoma minara ya *2G* lakini kwa maeneo ya mjini mengi yameshafikiwa na minara ya *3G* na *4G*. Iwapo bado kuna maeneo ya Mjini Tabora yanasoma minara ya *2G*, ninaomba kupitia Bunge lako Tukufu kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari nimwelekeze Mkurugenzi Mkuu wa *TCRA* apeleke timu yake ya wataalam kufanya tathimini katika eneo la Jimbo la Tabora Mjini ili kutambua ni kwa nini bado kunasoma minara ya *2G* ambayo katika maeneo ya mjini mengi hakuna changamoto kama hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shaffin Sumar, ajiandae Mheshimiwa Bulaya. Mheshimiwa Shaffin.

**MHE. SHAFFIN A. SUMAR:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo. Kwa kuwa tatizo la mawasiliano ni la nchi nzima na katika Jimbo langu la Uyui tatizo kama hili lipo na linasumbua sana katika Kata ya Ibili, Ibelamirundi, Ndono, Makazi na Bukumbi. Je, ni lini Serikali itapeleka wataalam ili waangalie maeneo ambayo yanafaa kuweka mnara waweze kuweka haraka iwezekanavyo ili wananchi waache kupanda miti kutafuta mawasiliano? (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Uyui kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba nichukue nafasi hii pia kumwelekeza tena Mkurugenzi Mkuu wa *TCRA* kutuma timu ya wataalam katika Jimbo la Uyui kuweza kufanya tathmini na kutambua changamoto zilizopo za mawasiliano katika jimbo hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza. Katika Jimbo la Bunda Mjini kata za pembezoni pia kuna changamoto ya mawasiliano kama Kunzugu, Bukole, Nyamatoke na Mihali. Ni lini changamoto hiyo itatatuliwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mbunge wa Jimbo la Bunda Mjini, Mheshimiwa Bulaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tuna mkakati maalum na mahususi ambao tunauandaa Wizarani na utakamilika hivi karibuni. Mkakati huu tunakusudia kuyafikia maeneo yote yenye changamoto za mawasiliano likiwemo Jimbo la Mheshimiwa Bulaya. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa kwamba katika mkakati wetu huu na siku si nyingi tutamfikia katika maeneo yake yenye changamoto na nimpongeze pia kwa jinsi anavyowapigania wapigakura wake wa Bunda Mjini. Kwa kweli wamechagua Mbunge mahiri. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Thomas Kampala Maganga.

Na. 144

**Ujenzi wa Chuo cha *VETA* Mlele - Katavi**

**MHE. THOMAS K. MAGANGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Chuo cha VETA Halmashauri ya Wilaya ya Mlele – Katavi?

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, ninaomba nijibu swali la Mheshimiwa Thomas Kampala Maganga, Mbunge wa Katavi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na ujenzi wa Chuo cha *VETA* cha Wilaya ya Mlele ambacho kinatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2026. Hadi sasa Serikali imeshatumia jumla ya Shilingi Bilioni 1.032 kati ya Shilingi Bilioni 1.6 zilizotengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa awamu ya kwanza. Mpaka sasa, ujenzi huo umefikia 73%.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga na kupokea fedha ili kuwezesha ujenzi wa chuo hiki kukamilika kwa wakati na kuanza kutoa mafunzo kama ilivyopangwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maganga.

**MHE. THOMAS K. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru na ninaomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kulingana na umuhimu wa chuo hiki, je, ni lini sasa Serikali itapeleka fedha ili kukamilisha ujenzi huo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kabla sijaja Bungeni, nilitembelea mradi huo wa ujenzi, mradi huo hauridhishi. Je, Waziri yuko tayari kwenda kujionea halisi ya mradi na kutoa msukumo ili mradi ukamilike kwa wakati?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako ninaomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze kwa ufuatiliaji wake juu ya maendeleo ya Chuo hiki cha Mlele, lakini pia nimpongeze

nimepata taarifa kwamba yeye ndiye Mwenyekiti wa Wabunge wapya katika Bunge hili. Kwa hiyo nimpongeze kwa nafasi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye majibu yangu ya awali, kwamba kati ya bilioni 1.6 ambazo zilizotengwa, bilioni 1.032 tayari zimeshatumika. Kwa hiyo bakaa iliyobaki siyo kubwa sana na Serikali imeshatenga fedha kwa ajili ya kumalizia vyuo hivi na kuanza ujenzi pia wa vyuo vingine. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Maganga kwamba, fedha zitaenda na chuo hicho kitamalizika katika awamu ya pili. Ahsante

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, niko tayari kwenda na kuangalia maendeleo ya chuo hiki.

**SPIKA:** Mheshimiwa Matiko, hana swali. Mheshimiwa Waziri ninakushukuru kwa majibu yako.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea na Wizara ya Madini, Mheshimiwa Engineer Chacha.

Na. 145

**Kuanzisha Kituo cha Kuongeza Thamani na Soko la Bidhaa za Dhahabu – Geita**

**MHE. CHACHA M. WAMBURA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Kituo cha Kuongeza Thamani na Soko la Bidhaa za Dhahabu katika Mji wa Geita?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuchukua hatua madhubuti kuimarisha uongezaji thamani wa madini katika Mkoa wa Geita ili kuhakikisha manufaa ya rasilimali madini yanabaki nchini. Kutokana na uzalishaji mkubwa wa dhahabu, mkoa huu umewekewa miundombinu muhimu ikiwemo kiwanda kikubwa

cha Kusafisha Dhahabu vya Geita *Gold Refinery* (*GGR)* na *African Eyes Refinery* na pia kuna viwanda vidogo vya teknolojia ya kisasa ya uchakataji wa madini ikiwemo mifumo inayojulikana kama *(CIP (Carbon in Pulp)/CIL (Carbon in Leach))* pamoja na Vituo vya Umahiri vya Lwangasa na Katente vinavyosimamiwa na *STAMICO*. Hatua hizi, kwa kuzingatia sheria na sera zilizopo, zimefungua fursa kwa wadau mbalimbali kushiriki katika soko la bidhaa za madini Mjini Geita ikiwepo masuala ya usonara.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi ya kiujuzi, kiuwekezaji na kisheria ili kuimarisha uongezaji thamani madini nchini. Aidha, Wizara kupitia Kituo chetu cha Jimolojia Tanzania *(*Tanzania *Gemological Center)* ambacho kiko Arusha) inaendelea kutoa mafunzo ya vitendo ya uongezaji thamani wa madini na kuandaa wataalam wa utengenezaji wa bidhaa zitokanazo na dhahabu, fedha na vito. Hivyo, nitoe wito kwa Mheshimiwa Mbunge kuwahamasisha vijana wa Mkoa wa Geita hususani Jimbo lake la Geita Mjini kuchangamkia fursa hizi ili kujiajiri, kuongeza kipato na kuchangia maendeleo ya Taifa. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Chacha.

**MHE. CHACHA M. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini kwa majibu yake mazuri, lakini niseme tu kwamba wote humu ndani tunajua kwamba tunazalisha dhahabu nyingi Tanzania na hususani katika Mkoa wetu wa Geita, lakini dhahabu yote hii tunai-*export,* tunaisafirisha kwenda nje bila kuitengenezea vifaa vinavyotokana na dhahabu. Tukiweza kutengeneza vifaa hivi kama pete, mikufu na vinginevyo ambavyo vinatokana na dhahabu tutaenda kuongeza ajira, mapato, lakini pia tutakuwa sasa tunatengeneza Tanzania tuna-*export*, tutategemea tutopata wageni, lakini tutapata watalii.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; je, Serikali ina mpango gani mahsusi wa kuhakikisha kwamba tunaanzisha kituo maalum cha utengenezaji hivi vitu ambavyo vinatokana na dhahabu ili basi tuweze kuhakikisha kwamba vijana na wajasiriamali wa Geita

wanaweza kuhusika moja kwa moja kwenye mnyororo huo wa utengenezaji wa vitu hivi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; endapo itatokea Serikali haina mpango wa moja kwa moja wa kuanzisha kituo hiki, je Serikali iko tayari kushirikiana na sekta binafsi au Halmashauri ya Manispaa ya Geita kuwawezesha kuanzisha vituo hivi, maana ninaamini kabisa kwamba kwenye Geita na Taifa hili litaenda kuwa na faida kubwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Chacha kwa maswali yake mazuri na pia nimkaribishe katika Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa sababu nina taarifa kwamba hivi karibuni amepata kuelekezwa awe Mjumbe wa Kamati hiyo. Ninajua kwamba ni *Engineer* mwenye uzoefu na tunahitaji kuvuna hazina ya elimu aliyonayo katika Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nijibu sasa maswali yake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, viwanda vya kuchakata madini na kutengeneza bidhaa za mlaji wa mwisho (*end user products*). Tayari zipo katika sehemu mbalimbali nchini kama nilivyoelezea kwenye majibu ya swali la msingi, lakini kwa upande wa huko Geita sasa na kwa sababu Mheshimiwa Mbunge anataka kujua hasa bidhaa zinazotokana na dhahabu ni kweli kwamba sasa hivi dhahabu nyingi inachakatwa, wanachoma, wanatengeneza zile *ground bars* na zinauzwa hivyo hivyo ila ni kwa Geita tu na baadhi ya maeneo mengine nchini, lakini tayari tuna viwanda vinavyochakata dhahabu na kutengeneza bidhaa za dhahabu.

Mheshimiwa Spika, moja ya mfano hai ambao upo na hata Wanageita wanaweza kwenda kujifunza ni Kiwanda cha *Banjul Limited* kilichoko Dar es Salaam ambacho kinafanya biashara ya kuchakata madini ya dhahabu na kuuza dhahabu nje kama wanavyouza wengine, lakini pia wanatengeneza vidani, mikufu,

pete, bangili, lakini siyo ya dhahabu tu na madini mengine mbalimbali ikiweko madini ya metali pamoja na madini ya vito.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia katika kujibu swali lake la pili kumwelekeza Mheshimiwa Mbunge, ashauriane na Halmashauri yake maana na yeye ni Mjumbe Halmashauri ya Geita siyo maskini, wakitaka kuanzisha kiwanda cha kuongeza thamani ya madini ya dhahabu na kutengeneza bidhaa za mlaji wa mwisho, sisi kama Wizara tuko tayari kutoa ujuzi na elimu kwa kuwaletea wataalam waweze kuanzisha kiwanda ambacho kitahakikisha kwamba dhahabu ile inatengenezewa bidhaa mbalimbali zinazoweza kutumika nchini na Watanzania wote, siyo lazima kuuza bidhaa ambazo zimechakatwa tu kwa asilimia Fulani.

Mheshimiwa Spika, tunaweza kutengeneza bidhaa za mlaji wa mwisho na wako wengi ambao ninapenda kuwapongeza wanaotengeneza bidhaa za madini ya vito hasa kule Arusha ambako kuna kile chuo chetu cha *TGC,* lakini pia kuna wadau mbalimbali katika mikoa mbalimbali nchini, Mererani pia wanafanya hivyo katika madini ya *Tanzanite* na Dar es Salaam kuna watu binafsi ambao wanajishughulisha na biashara hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sisi tuko tayari kama Wizara kuiwezesha Halmashauri ya Geita kwa kuwapa utaalam ili waweze kuanzisha kiwanda cha kuchakata madini au kituo kikubwa kama kile cha Tanzanite *City Center.*

**SPIKA:** Ahsante ameshakuelewa. Mheshimiwa Ngajilo

**MHE. FADHILI F. NGAJILO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kupewa nafasi hii kuuliza swali la nyongeza. Mkoa wa Iringa unasemekana una maeneo yenye madini. Ukienda mfano Ihomasa, Ihandutwa, Sinai, Ulata, Mtera, Kitonga, Image na maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Iringa. Swali, je, ni lini sasa Serikali wataifungua na kuipa kipaumbele Iringa ili mkoa huu ujulikane ni mkoa wa madini kwa kufanya *mining survey* lakini kutangaza maeneo yenye madini na kuwawezesha vijana kwa teknolojia ya kuchimba madini na kutengeneza mabilionea kutoka mkoa wa Iringa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri na nimjulishe tu kwamba Iringa nayo ni mikoa yetu ya kimadini, wana madini ya aina mbalimbali na nimpe ushauri kwamba atembelee Kituo chetu cha Jiolojia (*TGC*) pale *GST* kwa sababu kuna kitabu ambacho huwa kinahuishwa kila baada ya miaka mitatu, kinachoeleza madini yanayopatikana katika kila eneo la nchi yetu ikiwepo Mkoa wa Iringa.

Mheshimiwa Spika, hatuishii hapo tu, tuna wachimbaji wadogo wengi pale Iringa, eneo la Nyakavangala ambalo lipo katika Jimbo la Mheshimiwa Lukuvi, tayari ambako kuna wachimbaji wa dhahabu na madini ujenzi. Hivyo ni wajibu wetu kama Wizara kuendelea kutoa elimu kwa vijana ili waingie katika sekta hii kwa wingi, kwa sababu madini haya yanaenda kubadilisha sura ya uchumi wa wananchi wetu na vijana hasa ambao wanahitaji ajira.

Mheshimiwa Spika, kwa suala la *survey*, sisi kama Wizara ya Madini kwa maelekezo ya Rais tuko katika mchakato wa mwisho wa kununua ndege yetu wenyewe ya kufanya *survey,* lakini pia tuna wadau wa sekta binafsi ambao wameanza kurusha ndege, wameanza kurusha helikopta, wameanza pia kurusha na zile ndege nyuki katika kutafuta madini yalipo katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Tumeshafanya hivyo Shinyanga, wiki iliyopita na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa John Francisco.

Na. 146

**Ujenzi wa Uwanja wa Ndege Mwanza**

**MHE. JOHN F. NZILANYINGI** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa Uwanja wa Ndege Mwanza utakamilika ili uwe na hadhi ya Kimataifa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mpango wa Serikali wa kufanya maboresho makubwa ya Kiwanja cha Ndege cha Mwanza ili kuwa cha kimataifa umeanza. Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina unaohusisha ujenzi wa jengo jipya la abiria, upanuzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege, upanuzi wa eneo la maegesho ya ndege na ujenzi wa barabara za kiungio unaendelea.

Mheshimiwa Spika, ujenzi utaanza mara baada ya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kukamilika.

**SPIKA:** Mheshimiwa John Francisco

**MHE. JOHN F. NZILANYINGI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa majibu ya Serikali, lakini ninaomba sasa niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; ninaomba kufahamu, huo upembuzi yakinifu unahusisha kitu gani na utakamilika lini? Kwa sababu tarehe 28 Machi, 2024, Serikali ilisaini mkataba na mkandarasi anayeitwa Taifa *Civil Mining Limited,* mkataba ambao ulikuwa na zaidi ya thamani ya bilioni 29.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo ya Serikali, wananchi wa Nyamagana, nikiwemo mimi mwenyewe kama mwakilishi wao, ninapata mkanganyiko wa nini ambacho kinaendelea kufanyiwa upembuzi yakinifu, ilhali Serikali tayari imekwishasaini mkataba.

Mheshimiwa Spika, swali la pili; toka Serikali isaini mkataba huo, haijawahi kupeleka hata senti tano. Hivi ninavyozungumza, kwa taarifa nilizonazo, mkandarasi ameanza kuondoa vifaa vyake *site*. Ni lini sasa Serikali itapeleka fedha ili mkandarasi aweze kuendelea na kazi ya ujenzi wa uwanja? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI**: Mheshimiwa Spika, kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Nzilanyingi kwa ufuatiliaji wake wa karibu kwenye uwanja wetu huo wa Mwanza, lakini yeye Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote wa Mkoa wa Mwanza na Kanda ya Ziwa kwa ujumla, wanachama wa Chama Cha Mapinduzi na wananchi kwa ujumla. Kiko kilio kimoja ambacho wamekuwa wakikitoa kwa muda mrefu, ni lini uwanja wa Mwanza utapewa hadhi ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kufuatia maombi hayo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dr. Samia Suluhu Hassan, amepokea kilio hicho na amefanya usanifu, ametuelekeza kama sekta chini ya Waziri wetu Mheshimiwa Mbarawa tumefanya tathmini ya kina na kubaini kuwa, iko haja kubwa ya kuufanya uwanja kuwa wa kimataifa.

Mheshimiwa Spika, sasa mambo mazuri yanahitaji pia subira, nini kinafanyika kama nilivyosema? Mambo matatu; la kwanza Jengo lilopo kwa sasa, linatosha abiria karibu 400,000 – 500,000. Tunataka tufanye usanifu ili tuweze kujenga jengo kubwa litakaloweza kubeba abiria zaidi ya milioni mbili na laki tano. Ili ndani ya jengo, tuweze kuweka taasisi zote muhimu ambazo ni sifa na takwa muhimu kwenye uwanja wa kimataifa; Uhamiaji, Afya, pamoja na Maliasili na vitu vingine vingine. Mbili, *runway;* ili uwanja uweze kuwa wa kimataifa, ule upana wake hautoshi. Tunaongeza kutoka meta 45 mpaka meta 60 na ku-*maintain* urefu uliopo wa takribani meta 3,800.

Mheshimiwa Spika, la tatu, ni taa. Ule uwanja uliopo awali tulifikiri pengine zile taa zingetosha, lakini baada ya tathmini ya kina, inaonekana kabisa kwamba zile taa hazitatosha kwa sababu zilijengwa miaka ya 1970. Hivyo basi, tunataka tubadilishe taa zilizopo na kuweka za kisasa. Kwa sababu hiyo nimwombe Mheshimiwa Mbunge pamoja na Wabunge wote waweze kuwa na subira.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, ameuliza kwamba Serikali haikupeleka fedha ni kweli na jengo lililopo linafanya nini? Jengo lililopo sasa ambalo tulikuwa tumeshaanza ujenzi ambao tunashirikisha sekta binafsi tutalitumia kwa ajili ya *general aviation*. ndege ndogo, wale watu wa *premium,* ukiwa na ndege yako, utatumia jengo hilo. Lengo ni jema tu, kuhakikisha kwamba tunaupa hadhi ya kimataifa na inayostahili uwanja huo ambao unasafirisha bidhaa mbalimbali kutoka nchini kwetu minofu ya samaki, maliasili pamoja na utalii, kwa maana ya utalii kwa ujumla na kadhalika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Mwanyika.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa nafasi. Hitaji la Uwanja wa Ndege wa Njombe ni kubwa sana kutokana na uchumi wa Njombe, lakini ni mradi wa kimkakati, pia ni ahadi Rais, ni lini sasa ujenzi wa uwanja huu utaanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mwanyika kwa ufuatiliaji wake wa karibu sana juu ya Uwanja wa Ndege wa Njombe. Yeye na Wabunge wenzake wa Mkoa wa Njombe wanafanya kazi nzuri. Serikali imetambua na kuthamini umuhimu wa uwanja wa Njombe kama nilivyosema kwenye kubebea mazao kama vile parachichi na kadhalika na kwa sababu hiyo, Serikali inakwenda kujenga uwanja mkubwa. Ni hatua gani tuko mpaka sasa hivi?

Mheshimiwa Spika, tayari tulikuwa kwenye hatua ya kwanza ya kutafuta eneo, kwa sababu eneo la pale mjini halitoshi. Tayari viongozi wa mkoa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege wanashirikiana. Hatua ya pili tunayokwenda sasa ni kwa ajili ya kufanya usanifu ili tuweze kujua kiasi gani kinachohitajika uwanja utakaojengwa uweze kwenda sawasawa na hadhi ya Mkoa wa Njombe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kafiti, jiandae Mheshimiwa Bonnah.

**MHE. KAFITI W. KAFITI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Kutokana na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, bado sisi kama Mwanza na kama wakazi wa Jimbo la Ilemela, tunahitaji kujua huo upembuzi yakinifu utakamilika lini?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ukamilishwaji wa uwanja huu...

**SPIKA:** Mheshimiwa, swali ni moja tu.

Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI**: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kafiti Mbunge wa Ilemela alikuwa anajaribu kukazia hoja ile ile ya uwanja wa ndege na kimsingi yeye pale kwake hoja kubwa ambayo anaizungumzia ni upande wa fidia au namna ya kuweza kuondoa wananchi wa pale. Serikali ina dhamira ya kuufanya Uwanja wa Ndege wa Mwanza kuwa wa kimataifa. Ili uweze kuwa na sifa hizo, lazima kama kuna wavamizi waondolewe. Kwa hiyo, nimwombe tu awe na subira, tutamilisha muda siyo mrefu tutaanza kufanya kazi.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Bonnah ajiandae Mheshimiwa Kadogosa.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri ambayo inafanywa, Mkoa wa Dar es Salaam *especially* Kipunguni ambako Serikali imefanya kazi kubwa kuwalipa wananchi wa pale, lakini bado kuna wananchi ambao wanahitaji kulipwa ili waondoke. Je, ni lini Serikali itawamalizia hawa wananchi wa Kipunguni pesa zao ili waweze kuondoka maana hapo kuna mateso makubwa? Ninashukuru

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kujibu tena swali lingine la Mheshimiwa Bonnah, Mbunge wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa kazi ambayo alishaianza huko mwanzoni kwa ajili ya wananchi wa Kipunguni. Kama tunavyofahamu wananchi hawa wamekuwa wakidai fidia zao kwa miaka mingi sana, lakini ni Dkt. Samia Suluhu Hassan, mara baada ya kuingia na mpaka mwaka jana kati ya fedha walizokuwa wanazidai amekwishalipa bilioni 66 kwa wananchi karibu 717 kati ya 1,147. Nimwombe Mheshimiwa Bonnah na Wabunge wote wa Mkoa wa Dar es Salaam wavumilie, wale waliobakia watakwenda kulipwa kadri ya upatikanaji wa fedha Serikalini.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kadogosa.

**MHE. MASANJA K. KADOGOSA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa hii fursa. Serikali ilifanya tathmini ya uwanja wetu wa Simiyu eneo la Igegu na hiyo tathmini ilifanyika kwa takribani miaka minne iliyopita. Je, ni lini sasa Serikali itatoa fidia lakini vilevile kuanza ujenzi wa uwanja ule?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mshimwa Spika, ninampongeza Mshimiwa Kadogosa kwa kufuatilia Uwanja wa Ndege wa Mkoa wa Simiyu kwa sababu pia ni sera za Serikali kuhakikisha kwamba angalau kila mkoa unaweza kupata uwanja wa ndege.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Serikali imeshakamilisha usanifu wa uwanja huo na tumebaini kwamba tunahitaji eka karibu 3,386 na wananchi 700 kama na 92 ambao tumewatambua pale kiasi wanachodai ni shilingi bilioni 6.2. Nimwombe avumilie. Mara baada ya upatikanaji wa fedha tutaweza kwenda kulipa eneo hilo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Midimu na jiandae Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Mheshimiwa

Kadogosa ameuliza ila ninataka kukazia hapo. Ni muda mrefu tunauliza kuhusu ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Mkoa wa Simiyu na Uwanja ule ukikamilika watalii watakua wanashuka. Pale ni karibu kwenda Serengeti na Ngorongoro. Ni lini sasa uwanja huo utakamilika? Tunataka kauli ya Serikali kwa sababu ni muda mrefu eneo limeshatengwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa swali la nyongeza la Mheshimiwa Midimu ambaye anasisitiza umuhimu wa Uwanja wa Ndege wa Simiyu. Kama nilivyokwishakujibu pale mwanzoni kwamba tayari tumekwishaainisha kiasi cha fidia kinachohitajika shilingi bilioni sita pamoja na wananchi ambao tunatakiwa tuwafidie na eneo lenyewe.

Mheshimiwa Spika, niwaombe Waheshimiwa Wabunge, mpango wa Serikali ni mzuri. Ukiangalia miaka mitano nyuma na sasa ni tofauti. Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan imekwenda kujenga viwanja karibu vyote nchini. Ni maeneo machache sana ambayo hatujayafikia. Ukiangalia Kanda ya Ziwa peke yake ambapo Waheshimiwa wako huko: Shinyanga, Musoma, Serengeti (tunakwenda kuanza kujenga), Kyabajwa na Mwanza yenyewe. Ninaomba Ndugu zangu wavumilie, tunakwenda kufikia eneo hilo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, ningependa kumwuliza swali la nyongeza Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Naibu Waziri amesema lile jengo la Mwanza litabaki kama jengo la *general aviation* na lina mkataba wake na yeye amefanya upembuzi yakinifu kwa ajili kujenga jengo la *international.* Kama halivunjwi kwa nini mkandarasi anaondoka asimalizie lile jengo? Ninakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, tunaendelea na mazungumzo katika Uwanja wa Ndege wa Mwanza ikiwezekana kujenga kwa kupitia mwekezaji binafsi (Sekta ya *PPP)* tushirikiane na mjenzi. Kwa hiyo, nimwombe awe na subira tukikamilisha taratibu atapata taarifa nzuri zaidi.

**SPIKA:** Waheshimiwa tumemaliza maswali yetu na leo tuna hotuba tatu: ya Mipango, Fedha na ya Waziri Mkuu.

Tunao wageni wa Mheshimiwa Waziri Mkuu; kuna wageni wawili wa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba - Waziri Mkuu, haw ani Dkt. Jim Yonazi - Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu; na Dkt. James Kilabuko - Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni waliokaa Jukwaa la Spika; wapo wageni wa Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ambao ni Dkt. Tausi Kida - Katibu Mkuu; Dkt. Fred Msemwa - Katibu Mtendaji, Tume ya Taifa ya Mipango; Dkt. Mursali Milanzi - Naibu Katibu Mtendaji Mipango ya Taifa na Ndugu Angela Shayo - Mkurugenzi wa Mipango ya Kitaifa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni wengine wa Mheshimiwa Profesa Mkumbo ni wakuu wa Idara na Vitengo, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji pamoja na Wakuu wa Idara na Vitengo kutoka Tume ya Taifa ya Mipango. *(Makofi)*

Kuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wapo wageni watano wa Mheshimiwa Paul Christian Makonda - Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ambao ni viongozi wa dini kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Dotto Jasson Bahemu, Ndugu Baraka Willias, mfanyabiashara kutoka Kahama, Mkoani Shinyanga. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni 10 wa Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, ndugu zake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wapo wageni 29 wa Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, wapigakura wake kutoka Kata ya Chamazi, Mkoani Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga, wafanyabiashara kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, Ndugu Mudrick Amir na Ndugu Abdulkareem Mathew kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, jana baada ya Mwongozo wa Mheshimiwa Musukuma kwenye mitandao jioni zilitoka taarifa nyingi sana za kutumia lugha ambazo siyo za kistaarabu kwa kuwakashifu na kuwasema Wabunge ambao labda walifahamika hawajui kitu hiki. Ninataka niwaambie wananchi, tuwe na ufahari na Kiswahili. Tujivunie kuwa katika Bara zima la Afrika ni Taifa moja tu la Tanzania ambalo tuna lugha ya Taifa na wote tunazungumza lugha moja. Mnatumia mitandao kukashifu au kudharau na kusema kuwa wenzetu majirani wasije wakasikia taarifa hizi haipendezi na ni kujidhalilisha tu basi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ndugu Shingo ni Mbunge wa Dar es Salaam na mimi ninamjua na hana shida na Lugha ya Kiingereza. Binadamu hukutwa na shinikizo, ka-*panic,* ndiyo mara yake ya kwanza. Kuna maradhi mengine wote sisi hatujui mnatuona tunatembea nayo. Kuna *post-stress traumatic syndrome,* unajikuta tu unashikwa na hofu. Kwa hiyo, niwahakikishie wananchi na Wabunge, uwakilishi wetu kwenye nchi nyingine na kwa vile Kiswahili sasa kinatambulika kimataifa kutakuwa na *interpreters,* unasema Kiswahili yeye atatafsiri kwa lugha nyingine. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, siyo kila mtu anajua Kiingereza. Kuna mataifa ya Asia hawazungumzi Kiingereza, kuna mataifa ya *South America* hawazungumzi Kiingereza na kuna mataifa ya

Afrika yanazungumza lugha za kwao badala ya Kiingereza na vilevile wanasaidiwa kwa kutafsiriwa na watu maalum. Kwa hiyo, niwaombe sana tusiwe tunaponda kila kitu tu. Huna mahali pa kwenda zaidi ya Tanzania. Niwaombe sana ndugu zetu wa mitandao, vitu kama hivi havipendezi na wala havileti heshima kwa Taifa. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria kwa ajili ya Kufanya Marekebisho katika Sheria mbalimbali zipatazo 21 kwa Lengo la Kuondoa Mapungufu ambayo Yamejitokeza Wakati wa Utekelezaji wa Baadhi ya Masharti katika Sheria hizo *(A Bill for an Act to Amend Certain Written Laws in Order to Keep the Laws Updated with Some Challenges Observed in their Implementation)***

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria kwa ajili ya Kuweka Masharti ya Usimamizi wa Maslahi katika Dhamana za Mikopo za Mali Zinazohamishika, Kuanzisha Masijala ya Usajili wa Maslahi katika Mali Zilizotumika kama Dhamana, Kuainisha Masharti ya Utengenezaji Vipaumbele na Utekelezaji wa Maslahi katika Dhamana, Kuainisha Haki na Wajibu wa Wahusika wa Maslahi katika Dhamana ya Masuala Mengine Yanayohusiana na hayo**

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Miswada hii yote imeshasomwa kwa mara ya kwanza. Kwa sasa ninaelekeza Muswada wa kwanza wa *The Written Laws Miscellaneous Amendment* uende Kamati ya Katiba na Sheria na Muswada wa pili, Muswada wa Sheria wa Mikopo ya Dhamana ya Mali Zinazohamishika wa Mwaka 2026 utakwenda Kamati ya Bajeti.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MIPANGO**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu 2026/2027 - 2050/2051, Mapendekezo ya Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/2027 – 2030/2031) na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2026/2027**

**na**

**Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali katika Muda wa Kati ya 2026/2027 - 2028/2029.**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa leo tuna wachangiaji watatu. Mchangiaji wa kwanza ni Mheshimiwa Sigrada Wilhem Mligo, ajiandae Mheshimiwa Ado Shaibu na Mheshimiwa Subira. Watoa hoja pia wajiandae.

**MHE. SIGRADA W. MLIGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi hii ili niweze kuchangia kwa ufupi sana Mpango wa Maendeleo 2025/2050. Mimi nina mambo machache sana ambayo yamekuwa yakisumbua kwa muda mrefu sana. Kuna *issue* ya vijana na akinamama na hiyo mikopo ya 10%. Kuna changamoto kubwa sana kwenye hii mikopo na changamoto siyo kwamba fedha hazipo, lakini pia changamoto siyo kwamba wananchi wanashindwa kukidhi vigezo

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa ambayo nimeiona ni *complications* za namna ya kuipata hiyo mikopo. Hiyo mikopo imekuwa na *complications* nyingi sana. *Complication* ya kwanza walengwa kabisa watu wa chini hawaipati hiyo mikopo, lakini ukweli ni kwamba hiyo mikopo vinaundwa vikundi hewa vya watu wenye *access* ya kuifikia hiyo mikopo kwa kutanguliza watu ambao siyo walipaji na ndiyo maana ikija kusumbua, halmashauri zinapoanza kufuatilia zile fedha haziwaoni wahusika, ndiyo maana wanakutana na kitu kinaitwa vikundi hewa. Huo ndiyo ukweli, kwa sababu taarifa za hizi fedha haziwafikii watu ambao ni walengwa kule chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ushauri wangu kwenye huu Mpango ambao unaendelea ambao unahusisha na haya mambo pia; kuna mtu alishauri hapa, hizi fedha ziwe na mlango maalum. Nimeona sasa hivi Serikali imepitisha hela upande wa wanawake na watoto kupitia Waziri wa Mambo ya Wanawake na Watoto; pia na Vijana; kuna fedha zimepitia kwa Waziri wa Michezo na Utamaduni (Mheshimiwa Makonda); kuna fedha zimeenda huko *CRDB* na *NMB;* na kuna fedha zinapitia halmashauri. Hivi vitu vinatuchanganya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia masharti ya hizi fedha, Wizara ya Michezo ina masharti yake; halmashauri wana masharti yao na ukija hizi fedha za *NMB* zina masharti yake. Kuna watu wamesema ni fedha ambazo hazina riba. Ukiangalia ule mwongozo unasema zile fedha zina riba ya asilimia saba. Ushauri wangu, kwa nini Serikali isitoke na *format* ya pamoja ili kusiwe na lugha tatu utafikiri kuna Serikali saba kwenye nchi moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hizo fedha ambazo zinapatikana *NMB,* kwanza kuna mwongozo ulitolewa na Serikali kwamba watu wanaotakiwa kukopa hizo fedha ni watu ambao mtaji wao ni chini ya shilingi milioni nne. Ukiangalia hao watu maana yake ni watu ambao ni wajasiriamali na ninakumbuka kipindi cha Hayati Magufuli alitoa *formula* nyepesi sana kwamba watu ambao mitaji yao ni shilingi laki mbili, tatu, nne na tano (chini ya shilingi milioni nne) wawe na vitambulisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ni hii hii miaka 65, lakini ule mpango ule baada ya Mheshimiwa Magufuli kufariki ule mpango nao haupo. Wale wajasiriamali wadogo wadogo wamerudishwa tena kwenye shilingi elfu sita kila mwezi, kitu ambacho tunawachanganya watu. Unavyowaambia tena hawa watu wawe na leseni wakati ukiangalia sheria ya kodi inamtambua mfanyabiashara ambaye ana mtaji wa kuanzia shilingi milioni nne kwenda juu. Hawa watu wamesema wawe na mtaji wa chini ya shilingi milioni nne. Huyu *tax clearance* anaitoa wapi? *TIN Number* anaitoa wapi? Leseni ya biashara anaitoa wapi? Wakati huyu wamemchukulia kama ni mjasiriamali mdogo ambaye analipa ushuru wa halmashauri husika. Kwa hiyo, kuna *contradiction* ambazo zinafanywa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu, tuwe na *formality* iliyo wazi ambapo watendaji wa vijiji na mitaa watawaambia *direct* watu wao. Hizo hizo fedha, kwa mfano za halmashari, wale wakopaji wa vikundi wawe wamechapisha mpangokazi wao. Baadaye watu wamechapisha wameenda kukopa fedha wakawaambia hapana hatutaki mpango uliochapishwa tunataka mpango ambao umeandikwa kwa mkono. Halafu hizo hizo fedha wanakopesha hawa watu wenye ulemavu. Masharti waliyoyaweka kwa watu wa kawaida wameweka na kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mtu hawezi hata kutembea, yeye amekaa tu pale kutembea hawezi unamwambia atoke kule Makete, nilikutana na walemavu Mheshimiwa Festo wanatoka kilometa karibu kumi na kitu kwenda halmashauri kupeleka hizo *documents.* Masharti ni yaleyale tofauti yake ni kwamba mlemavu anaweza kukopa peke yake, lakini masharti ya mwanasheria, sijui iandikwe. Mtu haoni unataka aandike ataandikaje na asaini mwenyewe kwa mkono wake? Kwa hiyo, *issue* siyo fedha, fedha ninaamini zipo, *issue* ni *complications* za namna ya kuzipata hizo fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, sisi Njombe Mungu ametubariki sana. Ninapata shida kuona Taifa kama la Tanzania ambalo tumebarikiwa kila kitu eti tunakosa fedha. Tunakosaje fedha nchi ambayo Njombe pale wilaya zaidi ya nne zina madini.

Sisi kule Makete kuna madini, Ludewa kuna madini, Njombe Mjini pale kuna madini, lakini ukiangalia kwenye taarifa zenu nchi nzima wamefanya *survey* 16% tu ya sehemu ambazo tunamiliki madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi leo hii Njombe hatukutakiwa kuwa na miradi yenye miaka sita haijakamilika. Haikutakiwa Njombe tukose hela za kukamilisha eti Barabara ya Ludewa – Njombe. Mimi huwa ninatafakari kwamba, hivi kweli huwa tunakaa mezani na kutafakari kwamba hii nchi tumebarikiwa? Ile Njombe ile, tuna miradi ya maji 2008 imekwama. Njombe ambayo ukiitazama kila kona, kila baada ya kilometa moja unakutana na mto, kila baada ya kilometa unakutana na mto. Huku mto, huku mto na huko mto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kampeni nilitafakari kitu kimoja. Wananchi wamefanikiwa kutoa maji bondeni kwenda kwenye vipalila. Sisi kule tuna kilimo maarufu kinaitwa vipalila, viazi vya kumwagilia. Mwananchi ndani ya siku 10 ameshatega maji mtoni ameyapandisha juu kwenye mashamba yake eka 20.

*(Hapa kengele ya kwanza ililia)*

**MHE. SIGRADA W. MLIGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika zangu zimeisha?

**MBUNGE FULANI:** Endelea.

**MHE. SIGRADA W. MLIGO:** *Okay* sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikawa ninajiuliza inawezekanaje mkulima wa viazi tena darasa la pili anapandisha maji kutoka mtoni ndani ya siku kumi amesambaza kwenye shamba lake la viazi halafu Serikali ina mradi wa 2008 na haujakwisha mpaka leo! Hivi inawezekanaje? Nikagundua, unajua Mheshimiwa Musukuma kuna vitu anaongea lakini ukimsikiliza vizuri unakuta kuna *logic* ingawaje huwa tunamcheka kidogo. Iko hivi, unakuta mkulima wa kawaida ambaye hana shule ana maarifa kuliko sisi ambao tuna *PhD* na *degree*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikasema basi inawezekana tuwe tunajifunza basi hata kwa hao watu ambao wao hawakwenda shule ila ni wakulima. Kwa hiyo, ninavyozungumza hivi na ninaipa ushauri Serikali kwamba, tunavyokwenda kutekeleza hii mipango basi tuangalie hata ile miradi ambayo ilikuwepo toka enzi hizo za Kikwete na Magufuli. Kuna miradi hiyo Njombe labda kama hamna taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Mradi wa Maji unaitwa Igongwi wa 2008. Haya ukija kwenye *issue* nyingine, kwa mfano uwanja wa ndege, mimi nimekuwa Diwani 2015 niliukuta uwanja wa ndege upo kwenye mipango kwamba tunataka Uwanja wa Ndege Njombe. Sasa hivi Njombe tuna wawekezaji wakubwa sana wanahitaji hiyo ndege ili waweze kusafirisha mazao yao na kuwahi *issues* zao. Mtu wa Njombe unaweza ukamkuta amevaa ndala lakini ana *billions.* Kwa hiyo, kupoteza shilingi milioni moja kwenda Dar es Salaam akawahi *deal* la shilingi milioni 800 haoni shida. Njombe wanahitaji ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkatuambia Baraza la Madiwani litafute eneo, mwaka 2015 hiyo. Tukatafuta eneo, na lipo mpaka leo, lakini mkatuambia tusimamishe wale wanaopatikana katika maeneo ya karibu, na hilo eneo ambalo tumehama, sasa wasiendeleze maeneo yao. Maskini, tukawasimamisha watu wanaoishi karibu na uwanja wa ndege kwa hoja kwamba, tunataka kuupanua. Miaka zaidi ya mitano wanasubiri tupanue uwanja, hatujawahi kupanua. Baada ya hiyo miaka mitano kwisha tumerudi tena, tunasema aah, aah, hapa hatupanui, tumehama, tunaenda Uwanja wa Ndege Kibena huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninavyozungumza hivi, hii *issue* ya Uwanja wa Ndege wa Njombe aliyoizungumzia Mheshimiwa Deodatus siyo ya jana, labda kwa sababu hawa Mawaziri ni wapya. Mimi nimeingia kwenye Baraza la Madiwani mwaka 2015, nimeikuta. Kuhamisha Uwanja wa Ndege tumepitisha sisi, na eneo tumetafuta sisi. Kwa hiyo, ninashauri, tunaomba uwanja wa ndege haraka, siyo stori mpya. Ni miaka 18 sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninaishauri Serikali…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu muda umeisha, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ado Shaibu. Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, jiandae.

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge, Zima ninashukuru sana kwa kuniona ili na mimi nitoe mchango wangu juu ya mipango iliyowasilishwa mbele ya Kamati yetu ya Bunge Zima. Ni lazima nikiri kwamba, leo ni moja ya kati ya siku za kipekee sana kwangu. Hii ni kwa sababu, zaidi ya mwongo mmoja uliopita, nikiwa nafanya kazi ya kujitolea katika Kigoda cha Mwalimu Nyerere juu ya umajumui wa Afrika. Yuko bwana mmoja aliniita katika moja ya migahawa ya Jiji la Dar es Salaam. Bwana huyo alinipa mawazo yake kwamba, kwa kadiri anavyonifahamu anadhani ninaweza kutoa mchango fulani kwenye jamii iwapo nitajiunga na siasa ya vyama vya siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakiri kwamba, nilimkatalia kwa sababu zangu binafsi, lakini baadaye kutokana na bidii yake juu ya jambo hili, na tafakuri yangu ya binafsi, niliamua kumkubalia. Bwana huyo ndiye ambaye leo Wizara yake imeandaa mipango tutakayoijadili hapa sambamba na ile ya Wizara ya Fedha. Bwana huyo ni Mheshimiwa Prof. Kitila Alexander Mkumbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasimama hapa kwa kujiamini sana kwamba, licha ya utofauti wetu wa kiitikadi Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo hatarajii hata kidogo kwamba, mimi nitasimama mbele ya Kamati hii nikajikita kumsifia peke yake. Ninafahamu kwamba, Mheshimiwa Prof. atafadhaika iwapo mimi nitajikita katika kuonesha changamoto bila kuonesha majawabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo siasa ninayoifahamu, hiyo ndiyo siasa ninayoitamani, na hiyo ndiyo siasa ninayoiota. Siasa ya kupingana kwa hoja bila kugombana, siasa ya kupishana bila kuumizana, siasa ambayo ninaamini siku moja isiyo ya mbali, siasa ya namna hiyo itakita mizizi tena katika duru za kisiasa za nchi yetu, ili kwa pamoja tuweze kutoa mchango wetu wa kuijenga nchi kwa upendo na mshikamano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa kwanza juu ya mipango yetu, kwa sababu, mawazo mengi yametolewa hapa na sitaki kurudia; la kwanza, ni mpango wowote ni lazima pia, utazame vihatarishi vya utekelezaji wa mpango ule. Mimi ninaona mpango haujatazama kwa kina vihatarishi vya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifuatilia siasa ya dunia hivi sasa mwenendo wa mambo katika siasa za Kimataifa unakuonesha kwamba, kuna mabadiliko ya kasi sana miongoni mwa Mataifa, hasa juu ya sera zao za mahusiano ya kimaendeleo na kudorora kwa nafasi na ushawishi wa majukwaa ya Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo linatutaka tuchukue tahadhari hasa katika kuhakikisha tunaweka vizuri masuala yetu ya ndani. Kama hatuweki vizuri masuala yetu ya ndani yatakayotufanya tuzalishe vizuri kwa utulivu, tukawa *focused,* tunaweza kujikuta tunapata changamoto katika *financing* ya mipango yetu na tukajikuta tunajikita katika kuwaumiza Watanzania kwa kuwabebesha mzigo mkubwa wa kodi ama kuingia katika mikopo ya kibiashara yenye masharti magumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninarudia rai yangu, tutengeneze nyumba yetu vizuri, tujenge mshikamano wa Kitaifa, tuweke mazingira mazuri ya kisheria, kikatiba na muafaka wa Kitaifa utakaotufanya mipango yetu ya uzalishaji. Kimakusanyo inabaki kama ambavyo tumeipanga, hilo ni jambo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili. Mipango yetu inasema kwamba, sekta binafsi itakuwa ndiyo *engine* ya utekelezaji wa mipango ile. Kwenye *financing* ya mipango yetu inasema kwamba, 70% itakuwa kwa sekta binafsi na 30% kwa

sekta ya umma. Ninaunga mkono rai iliyotolewa na Wabunge wengi kwamba, ni lazima tuendelee kuweka mazingira wezeshi yatakayoifanya sekta binafsi iweze kushamiri na itoe mchango wake katika uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi bado ninadhani hatuja-*define* na hatujaipambanua sekta binafsi tunayoitaka. Ni lazima tujiulize maswali magumu, sekta binafsi tunayoitaka sisi ni sekta gani? Je, ni sekta ya wachuuzi wa kigeni wanaopambana na wajasiriamali Kariakoo? Au ni sekta binafsi isiyozingatia utu, mazingira na maslahi mapana ya Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu, ni lazima tuiongoze sekta binafsi. Sekta binafsi isiyopangiliwa, sekta binafsi isiyoongozwa, haiwezi kuwa *engine* ya uchumi, itakuwa ni bomu linaloangamiza uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu, nimesoma Mipango hii, nimeangalia maeneo ya kielelezo, programu za kielelezo, ziko programu 14 na nikajaribu kuchambua. Nimeona katika kila programu tuna miradi ya kimkakati, kwa maana ya *flagship projects*. Tuna hatua kadhaa za kuchukuliwa na tuna Mipango mbalimbali. Hii maana yake ni kwamba tuna makumi na makumi ya masuala ya kuyafanyia kazi. Nimeangalia katika mpango wa muda wa kati, nimeona tuna miradi saba ya kielelezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwasi wangu ni kwamba Tanzania haijawahi kuwa na uhaba wa mipango tangu tupate uhuru, kwa maana ya Tanganyika na Mapinduzi ya Zanzibar. Changamoto yetu kubwa ni utekelezaji wa mipango tunayojiwekea. Nina wasiwasi tukipata *shock* yoyote katika Mipango, baadhi ya Mipango hii itapewa kipaumbele na baadhi itawekwa kapuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni lazima tuwe na Mpango fulani ambao tutauita, Mpango wa Kufa na Kupona. Kwamba, hata tukipata shida yoyote, kama Taifa, hili eneo ndiyo kipaumbele chetu namba moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siyo mchumi, lakini maoni yangu ninaomba Mradi wa Mchuchuma na Liganga ndiyo uwe wa kufa na kupona kwa sababu, Mchuchuma na Liganga ndiyo *drive* ya mapinduzi ya viwanda vya Tanzania kama tunataka kuhama kutoka katika maendeleo bandia ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunasema tuna maendeleo ya viwanda vya kuunganisha magari. Kwa maoni yangu, yale siyo maendeleo halisi ya viwanda, tena tusipokuwa makini unaweza kukuta ule ni uchochoro wa watu kuikosesha mapato Serikali. Yaani unakuta mtu vipuri vyote 100% anaagiza kutoka nje, anapata misamaha ya kodi, halafu akishaunganisha bila kujali ajira gani anazalisha sisi tunasema hayo ni mapinduzi ya viwanda. Mapinduzi ya kweli ya viwanda yataletwa na uzalishaji wa chuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri Mwenyezi Mungu ametupa chuma na makaa ya mawe hapo hapo, Mchuchuma na Liganga. Suala lisilosemwa sana ni palepale Mchuchuma na Liganga kuna madini ya kimkakati ya *titanium* na *vanadium,* ambayo yana thamani kubwa zaidi kuliko hata hicho chuma. Kwa hiyo, Mradi wa Mchuchuma na Liganga na Mradi wake shikizi wa Reli ya Kusini, kwa maana ya Reli ya Mtwara mpaka Bandari ya *Mbamba Bay,* ambao utakuwa na Tawi lake la Mchuchuma na Liganga uwe ndiyo mradi wa kufa na kupona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika neno langu la kuhitimisha, nimejipa *homework* ya kwamba, kila nikisimama nitakuwa ninakumbusha juu ya Katiba Mpya. Leo ninakumbusha tena kwamba, Katiba Mpya ndiyo funguo ya muafaka wa Kitaifa. Mchakato wake uanze mara moja, uwe wazi, ili wadau wote waweze kushiriki.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Subira. Waziri wa Mipango, jiandae.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi asubuhi ya leo na mimi kuwa mchangiaji wa mwisho wa taarifa ambazo zimewasilishwa ndani ya Bunge hili Tukufu. Hii imetokana na maono yako licha ya kwamba, ilihitajika tujadili Novemba, lakini uliona Bunge hili la Januari – Februari tujadili Mipango ya muda mrefu, Mipango yetu ya miaka mitano ijayo na mapendekezo ya Mpango mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru Mungu. Nakupongeza na kuwapongeza waliowasilisha taarifa mbalimbali, akiwemo Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na pia, Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitajielekeza kwenye programu za kielelezo, na hasa kwenye Mji wa Ekolojia ya Bahari ya Usafirishaji wa Kimataifa, Bagamoyo. Kwa nini nimeona niliunge mkono hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa sababu, baada ya kuona mapinduzi makubwa yaliyofanywa katika uboreshaji wa bandari zetu, Bandari ya Dar es Salaam na ya Tanga, namna ambavyo zimechangia ongezeko la mapato, kwa taarifa inavyosomeka, Bandari ya Dar es Salaam baada ya kuboreshwa na kuweka mbia *(DP-World)* imeongeza mapato kiasi cha shilingi trilioni moja na bilioni 200 zinakusanywa kutoka shilingi bilioni 800 iliyokuwa inakusanywa kila mwezi na Mamlaka ya Mapato ya Tanzania *(TRA)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaamini mradi huu ambao una miradi shikizi nane, na ni kwa mara ya kwanza kwa kweli hatua hii. Alipokuja Mheshimiwa Waziri Kitila katika ile miradi shikizi, miongoni mwao likiwemo eneo la viwanda na kuwakabidhi wawekezaji saba, lakini niliwiwa na hatua ya Serikali ya kuwawezesha hawa wawekezaji kuwapunguzia gharama ya ardhi kwa kuwapa hati bila ya ununuzi. Hatua hiyo imekuwa kivutio na ni mara ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ombi langu ni kama nilivyochangia siku za nyuma kwamba, kwa kuwa mradi huu utakuwa na miradi shikizi ikiwemo reli ya kisasa, ikiwemo upanuzi wa barabara ya Tegeta – Bagamoyo kwenda Tanga njia nne, ikiwemo barabara ya lami, ikiwemo pia na kufangamanisha eneo la viwanda lililojengwa kwa maono ya Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Awamu hii ya Sita, Kwala, na limeanza kufanya kazi na tija yake tunaiona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali katika kuhakikisha kwamba hii miradi ya kielelezo inaenda kutekelezwa, ihakikishe wananchi wa maeneo hayo, yale mahitaji yao, ikiwemo fidia na hapa ninaisemea lile eneo la Liganga na Mchuchuma, wameshakamilisha. Hata hivyo, bado eneo la Lindi la *LNG,* maeneo haya ya Bagamoyo na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, katika uwezeshaji kuhakikisha tunafikia uchumi wa kati wa kiwango cha juu, na uwezeshaji wa wananchi, kama ambavyo hii mipango imesema, ninaishukuru Serikali, imekuwa ikifanya tathmini, hususan katika suala zima la mikopo ya halmashauri. Tulikotoka ni mbali, tulikotoka tulishuhudia mikopo hiyo ikipelekwa kwenye vikundi hewa na ndiyo maana Serikali ilisimamisha kwa kipindi cha mwaka mmoja ikaja na tathmini, ikaja imejipanga vizuri. Kana kwamba haitoshi, imekuja na mfumo sasa wa kuomba mikopo hii kupitia mtandao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu katika hili, tumeona ziko fedha tumetenga katika halmashauri, katika dhima ile ile ya kumwezesha mwananchi na katika hatua ile ile ya kuzalisha ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali ifanye mfumo ule kuwa rafiki. Mafunzo kwa wananchi wetu: wanawake, vijana na watu wenye ulemavu na hasa hawa Maafisa Maendeleo ya Jamii katika maeneo yetu mbalimbali; uwepo wa vifaa vya TEHAMA katika halmashauri zetu na maeneo ambayo yatakuwa rafiki, ili makundi haya yaombe hii mikopo isiyokuwa na riba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, ninaona hii hatua, tumeanza utekelezaji wa miaka hii mitano ya Mpango huu kuelekea 2026/2027 – 2050/2051 pale ambapo tumeona utoaji wa shilingi bilioni 200; jana tumemwona Mheshimiwa Waziri Mkuu akiwa mgeni rasmi amekabidhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaomba katika utekelezaji wa hizi shilingi bilioni 200 za Mheshimiwa Rais, ambazo zimetolewa, na ameonesha anatenda, kuwe na mpango mahsusi, tujue kila wilaya ni benki gani zitahusishwa? Wizara zinazohusika zisimamie kikamilifu, ili kusiwe na usumbufu wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya hizo fedha, tumeona namna gani Serikali imejipanga, hata kupitia hizo fursa nyingine, kwenye benki mbalimbali. Ufafanuzi ambao umetolewa leo na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, hata maelekezo ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, kuhakikisha kwamba urasimu unatolewa, ili ahadi zilizotolewa zitekelezeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya hilo pia, tumeona Mpango huu wa miaka minne utahitaji shilingi trilioni 474, sehemu ya 70% ni Sekta Binafsi. Ninaungana na Waheshimiwa Wabunge waliosema ni namna gani Serikali iende kusimamia mkakati ule wa *Blueprint*, ili uweze kuleta tija. Pia, kuendelea kuweka vivutio vile ambavyo vina tija zaidi, kuendelea kupanua wigo wa walipa kodi, kuendelea kuiwezesha Mamlaka ya Mapato Tanzania, ili lengo la Serikali la 30 ya kuwezesha mipango hii litekelezeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kuendelea kuhakikisha inatumia ile taarifa ya Sensa ya Mwaka 2022 ambayo ilikuwa ya aina yake, ilihakiki majengo yetu, ambayo nayo ni miongoni mwa chanzo cha uhakika. Vilevile, Serikali kupitia mamlaka zake mbalimbali, kubuni vyanzo vipya vya mapato, ili tuweze kuratibu na kusaidia mipango hii kutekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Niseme wazi, tunapoenda kwenye Mpango mwingine wa Miaka Mitano, tunajivunia mafanikio ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo ambapo mafanikio yameainishwa hapa, katika sekta mbalimbali. Tunawiwa na kuona sasa Serikali imekuja na miradi ya

vielelezo, imekuja na miradi shikizi na ni mipango ya aina yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta nzima ya madini ninaipongeza Serikali yetu na ninaipongeza Serikali na Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu, kwa mujibu wa Katiba, yeye ni sehemu ya Bunge. Bunge lina sehemu mbili, Rais na Bunge lenyewe. Kwa hiyo, tuna kazi ya kuishauri na kuisimamia. Sasa mtu unayemshauri, ukiona mambo yametekelezeka, ni wazi lazima utampongeza na kumtia moyo, lakini utaweka mambo mengine Mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachotaka kusema kwenye suala zima la madini, tumeona namna gani Serikali kupitia wawekezaji binafsi imeanza ku-*support* jambo la kurusha ndege na kufanya uhakiki kutoka eneo la 16% kuelekea eneo la 50% mwaka 2030. Ni imani yangu mipango iliyoko itatekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Serikali kwenye suala zima la sekta wezeshi na masuala ya nishati namna ambavyo imejipanga, uwezeshaji, uzalishaji wa umeme na kadhalika. Ninaamini Mpango huu utatekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, ni namna watakavyoendelea kuwajibishana katika kusimamia Mipango hii, namna ambavyo imejipangia Serikali hatua kwa hatua, uwasilishaji wa taarifa za Mawaziri miezi kadhaa, taasisi nyingine na Tume yenyewe ya Mipango, itakayoenda kusimamia ni kiasi gani mipango hii inatekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa fursa hii. Ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Kitila Mkumbo, tutaendelea kuunga mkono na tutaendela kushauri na kuisaidia Serikali na kuona namna gani Mpango huu wa Miaka Mitano tunaouanza safari, unatekelezeka kwa ufanisi na dalili tumeziona kwa sababu kazi imeanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. NABIL AHMED ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja ya Dira ya Maendeleo, kweye Wizara ya Fedha. Wizara ya Kilimo imewekeza fedha nyingi kwenye miradi mbalimbali ikiwemo umwagiliaji, vifaa vya kupimia udongo, matrekta na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukasema ili tuanzishe viwanda lazima tuzalishe malighafi ili viwanda hivi viweze kujiendesha na mdau mkubwa ni sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili la sekta binafsi kuna mambo matatu:-

(i) *Exchange rate;*
(ii) *World market price for commodity (kahawa, pamba, etc);* na
(iii) *Service levy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunaanza msimu na *rate* ya shilingi 2,700 kwa *USD* moja, *rate* ya dola haipo *stable,* inakuja kushuka hadi shilingi 2,480 kwa dola na hapo alishasaini mkopo wa *USD* milioni 10; hapa amepata hasara ya *exchange rate*. Anakuja kupata hasara nyingine kwenye soko la dunia ikiwa bei ya zao kushuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, linapokuja suala la *service levy*, halmashauri zetu zinakusanya kodi hizi kwa *turn over. Turn over* hii inaingiza mkopo kutoka benki na riba zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri Wizara ya Fedha iangalie namna ya kuangalia ili *service levy* iweze kuwa-*charged* (kukusanywa) kutoka kwenye faida ya kampuni na sio *turn over.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Mipango, jiandae Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze maelezo yangu kwa kuhitimisha kwa shukrani. Kwanza nakushukuru sana wewe pamoja na wasaidizi wako, kwa jinsi ambavyo mmendesha mjadala huu kwa umahiri na umakini wa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa Mbunge wa Dar es Salaam tunajivunia kuwa na wewe, Spika wetu mwema, rahimu sana, mtu *very simple, but not simplicity*. Ukimkuta Kariakoo kule anakuwa kama Mbunge wa Ilala tu. Tunakushukuru sana Spika, lakini mimi nikiwa natoka Singida pia najisikia nimewekwa katikati ya ulinzi wa hali ya juu. Nikiwa Dar es Salaam, ninaye Spika, nikienda Singida ninaye Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, narudia kuishukuru sana Kamati ya Bunge ya Bajeti kwa uchambuzi wao makini sana, na jinsi walivyoibua maeneo mapya katika mapendekezo yao. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati mnaoongozwa na Mheshimiwa Mashimba Ndaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango. Hakuna shaka kwamba siku hizi tano, Bunge lako hili limethibitisha kwamba humu ndani unao Wabunge mahiri kwa kuzingatia michango yao. Ilikuwa ni michango ambayo ni *very high quality, to say the list,* nashukuru zaidi kwamba ni rahisi sana kuorodhesha makosa, lakini ni ngumu sana kupendekeza majawabu juu ya changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninyi mmekuwa tofauti katika michango yenu, hamkuishia tu kulalamika, mmeonesha changamoto, lakini mmeonesha majawabu ya changamoto ambazo mmezitoa. Kwa hiyo, tunawashukuru sana na tumeona kabisa kupitia mjadala huu ni wazi kwamba vipaumbele ambavyo mmeviibua ndivyo vipaumbele ambavyo vipo ndani ya Mipango na tunashukuru kwamba Mipango ambayo tumeileta hapa imeakisi matakwa ya wananchi kwa jinsi michango yenu ilivyokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla wake sekta ambazo zinazalisha fedha, watu wote hapa wamezungumzia umuhimu wa kuwafanya Watanzania wapate fedha, na tumeeleza sekta nyingi, lakini nifanye *summary* kidogo. Tunazo sekta tatu tu kimsingi ambazo hapa nchini kwetu na duniani kote zinaweza kuzalisha fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna shaka sekta ya kwanza ni sekta ya kilimo. Kitu kipya ni kwamba, Mpango unazungumzia kilimo cha biashara, na tumefanya vile kwa sababu tatizo ambalo tumekuwanalo la msingi limekuwa ni kuwa na kilimo cha kujikimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka tutoke hapo twende kwenye kilimo, tupate chakula, kwa maana ya kuhudumia tumbo, lakini tupate fedha kwa maana ya kuwa na fedha mfukoni. Kwa hiyo, kilimo cha tumbo na kilimo cha mfuko ili watu wetu wapate fedha kutoka kwenye kilimo, hicho ndicho kitu kikubwa sana ambacho Mpango umeeleza hapa na ninyi mmesema aina mbalimbali ya mazao na kadhalika na kadhalika. Kwa hiyo, ni eneo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya pili, ni suala zima la ufundi. Teknolojia na uzalishaji viwandani. Kwa hiyo, huku ndiko ambako tunamaliza rasilimali kutoka kwenye kilimo, zinaingia kule, zinafanyiwa *Agri processing,* zinabadilisha kilimo mazao yale kuwa bidhaa, unaongeza thamani, unaweza ukaiuza. Tunazo rasilimali mbalimbali hapa za kupeleka wenye viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili ni eneo kubwa, hapa pia ndiyo tunaongelea habari za ile inaitwa *knowledge-based industries* kama vile *IT* na kadhalika, ubunifu wote unaingia hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni huduma *(service)*. Hili ni eneo ambalo linabeba watu wengi sana. Tunazungumzia hoteli, usafiri, kwa hiyo, ukiona bodaboda, mabasi yote, hiyo ni sekta ya huduma. *Music* ambao sisi tumebarikiwa kuwa na muziki sana hapa Tanzania; muziki ni sekta ya huduma, na ni sekta muhimu ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za kitaalamu kama afya, elimu, zote hizo utalii. Huduma za dini, tunapowaona Wachungaji, Hashehe, na wenyewe wanachangia, ni huduma katika sekta ya uchumi. Uuzaji wa bidhaa, TEHAMA zote hizo ni huduma. Kwa hivyo, sekta zote hizi tunazizingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichopo katika *modernization* ni kwamba, uchumi unavyokua watu wanaanza ku-*move* kutoka kwenye kilimo kwenda kwenye viwanda kwenda kwenye huduma, ndivyo ilivyo *trend* duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunatarajia hapa kwetu, na kwa kweli, takwimu za mwaka 2024 zinaonesha kwamba idadi ya Watanzania ambao wanategemea kilimo kwa sasa imepungua kutoka 65% mwaka 2021, mwaka 2024 inaonesha kwamba ni 54% na tunatarajia katika kile kipindi cha utekelezaji wa ilani itashuka, itafika 50%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo haimaanishi kwamba uzalishaji utashuka, uzalishaji utaongezeka, isipokuwa watu wengi zaidi unapokuza viwanda, unapokuza sekta ya huduma, wanazidi kumezwa kule, na *GEN-Z* tulionao ni watu ambao wanapenda zaidi kwenda kwenye huduma na kwenda kwenye viwanda. Kwa hiyo, ni eneo ambalo tumeliweka hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati ambayo tunayo ni kwamba siyo kila nchi duniani zina maeneo hayo matatu. Zipo nchi ambazo zina huduma pekee. Ukienda Japan, kwa mfano huzungumzii kilimo kwa sababu hawana eneo la kulima. Sisi ni miongoni mwa nchi tatu ambazo maeneo yote matatu tunayo. Tunaweza kulima, tunaweza kufanya viwanda na tunayo sekta ya huduma. Kwa hiyo, ni eneo ambalo tunalo na ni *advantage* na mipango imejaribu kuainisha ni namna gani hayo mambo matatu yanazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi lazima tu-*balance* uzalishaji na ulaji, mambo yote mawili haya; uchumi lazima uzalishe, na pia uchumi lazima watu wale. Sasa ndiyo umuhimu wa kukuza *middle class*. Ndiyo maana kwenye mpango, tunazungumzia kukuza

*middle class*. Hakuna sababu ya kujenga hoteli kama hamna walaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitaka kuona *middle class* inakua kwa kiasi gani, zungukia kwenye migahawa. Watu wamejaa. Ukikuta watu wawili, mmoja ujue hapo ni changamoto. Kituo kimojawapo angalia, je, kwenu hapo, katika nchi yenu, kuna *MacDonald?* Kuna *KFC?* Kama hizo hazijaja, maana yake bado *middle class* ipo chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, moja ya eneo tuliloweka mkazo mkubwa ni kukuza *middle class,* lengo ikiwa ni kukuza pia uchumi wa ulaji kwa maana ya *consumption*. Kwa sababu, uzalishe na walaji uwe nao, kwa kuwa soko la kwanza ni soko la wananchi wako mwenyewe. Kwa hiyo, ni eneo ambalo tumeliwekea mkazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe tu ufafanuzi wa maeneo kama mawili, matatu, ambayo Waheshimiwa Wabunge wameeleza hapa. Kwanza ni umuhimu wa sekta ya kilimo, hili hakuna shaka. Niseme kwamba pamoja na changamoto ambazo wameziainisha, tusisahau katika utekelezaji wa mpango wa miaka mitano huu, tumepiga hatua kubwa sana hususan tangu mwaka 2021, Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia aliweka mkazo na kipaumbele kikubwa sana kwenye kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza kuangalia takwimu zifuatazo; kwa mfano, bajeti ya Wizara ya Kilimo peke yake, imeongezeka wa 324% kutoka shilingi bilioni 294 mwaka 2021/2022 hadi kufikia shilingi trilioni 1.25, imepanda mara 324. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia angalia upandaji wa mbegu bora, Waheshimiwa wamezungumzia mbegu bora hapa, tulikuwa na tani 50,000. Sasa tunazungumzia tani karibia 80,000 hatujafikia lengo, lakini hatua kubwa imepigwa, matumizi ya mbolea yameongezeka tani 363,000 mpaka tani 850,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la umwagiliaji wetu wengi wamezungumzia hapa. Kwa muda mrefu tulikuwa na lengo la kufikisha hekta milioni moja ya umwagilliaji, ndiyo lilikuwa lengo

kwenye Mpango wa Maendeleo uliopita. Kwa miaka yote ilibaki kwenye hekta 410,000, lakini ninavyozungumza leo tumeshafikisha hekta 983,466.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, bado safari ni ndefu, lakini msisahau pia tumepiga safari kubwa sana ukilinganisha na ambapo tumetoka. Lengo ambalo tumejiwekea kwenye Mpango uliopo ni kufikisha hekta milioni tano ifikapo mwaka 2030/2031. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi, ajenda ya kilimo ni ajenda ya kudumu kwa CCM na ni kipaumbele mama kwa Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ukitaka kuthibitisha hilo, tazama amewateua makada bora kabisa. Waliokabidhiwa sekta ya kilimo ni waliokuwa Makatibu Wakuu wa Chama Cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo, kakabidhiwa Ndugu yetu Mheshimiwa Daniel Chongolo, moja ya Makatibu Wakuu bora wa CCM. Wizara ya Mifugo na Uvuvi, amekabidhiwa Ndugu yetu Mheshimiwa Dkt. Bashiru Ally Kakurwa ambaye ni moja wa Makatibu Wakuu bora wa CCM. Hii siyo bahati mbaya, ni kuonesha kwamba Rais ameweka mkazo na kipaumbele kikubwa sana katika sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya pili, Waheshimiwa Wabunge, wameeleza haja ya kutunga sheria ya ugatuaji. Tuseme ni kweli, kwa muda mrefu tangu 1998 ugatuaji umeendeshwa na tamko la kisera la ugatuzi la mwaka 1998. Serikali imeshaamua pamoja na mafanikio yaliyopatikana, tunaenda kutunga, kuandaa Sera ya Taifa ya Ugatuaji. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI analifanyia kazi hili, na baada ya hapo, tutakuja na Sheria ya Ugatuaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana tuzingatie kwamba, Mpango Elekezi na Mpango wa Miaka Mitano umeainisha hatua za kuimarisha Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa sana, lazima tukubali kifikra, kimatendo, kimwenendo na kisheria kusogeza madaraka

na mamlaka na fedha kwenda Mamlaka za Serikali za Mitaa. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haitawezekana kuleta maendeleo katika nchi hii kutokea Dodoma. Maendeleo lazima yatokee kwenye *Local Government* kwa sababu ndiko kuliko na wananchi. Haiwekezekani tulivyoweka kwenye Mpango tunatarajia ifike mahali Bunge lako hili lisijadili habari ya kujenga vituo vya mabasi, Bunge hili lisijadili habari ya kujenga madarasa, Bunge hili lisijadili habari ya matundu ya vyoo, mambo haya yafanyike kwenye *Local Government. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tujadili namna ya kwenda *space* kule. Kwa hiyo, ili tufanye hayo, lazima tuimarishe *Local Government*. Tusipoimarisha, tutakuwa tunajadili kero hapa. Kuna tofauti ya kujadili kero na maendeleo. Kero zishughulikiwe kwenye *Local Government* na Bunge lijadili mambo ya msingi ya maendeleo. Kwa hiyo, hili ni eneo ambalo lazima tulizingatie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni mchango wa sekta binafsi. Tunaungana, ile tumeweka 70 na 30 imefanyiwa utafiti mkubwa. Hata sasa, tunapimaje mchango wa sekta binafsi? Tunaangalia ile Wazungu wanaita *Gross Fixed Capital Formation* unavyounda ile mitaji hata sasa, kwa miaka mitano 2020 - 2024 utaona kwamba jumla tuliweza ku-*raise capital* ya shilingi trilioni 344.2, sekta binafsi shilingi trilioni 241 na sekta ya umma shilingi trilioni 103. Kwa hiyo, tayari shilingi trilioni 201, hiyo ni 70% ya *all the capital formation in the country*. Kwa hiyo, tayari sekta binafsi inachangia katika mitaji yote ya uwekezaji nchini 70% na sekta ya umma *only* 30%. Kwa hiyo, tayari hiyo ambayo tumeweka inaweza kutekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni suala la kutunga sheria na taasisi ya ufuatiliaji na tathmini. Sheria ambayo mmeitunga hapa ya Tume ya Taifa ya Mipango Sura ya 127, moja ya jukumu lake ambalo imepewa ni kubwa, ni suala la *M&E*. Suala hapa ni utekelezaji. Taasisi ndiyo hiyo imekabidhiwa jukumu, Mwenyekiti wake ni Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha muhimu, tusimamie utekelezaji na Wizara za kisekta kazi yake kubwa itakuwa ni sera, usimamizi na vilevile *M&E.* Mambo mengi yafanywe katika shughuli za chini, na miradi siku ambayo wameizungumzia hapa nimemsikia Mheshimiwa Ado, hili suala la *LNG*, suala la Liganga Mchuchuma, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan baada ya takribani zaidi ya miaka 20, hii miradi amesha-*unlock*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *LNG* nimeeleza hapa, tupo hatua za mwisho, Liganga, Mchuchuma imeshalipwa fidia, *GNT* wanamalizia majadiliano, miradi hii inaenda kuanza. Ameshaanza kuikamilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nieleze tu kwamba Mipango ambayo tumewasilisha hapa ambayo ni nyenzo za utekelezaji wa dira, Mipango hii imeandaliwa na Watanzania, wataalam wetu wa ndani ndiyo wameandaa. Hata hivyo, ili kuhakikisha kwamba nyaraka hizi zinakidhi viwango vya Kimataifa, zimefanyiwa mapitio na taasisi za tafiti za ndani na nje ya nchi. Kwa hiyo, tulifanya utafiti, lakini walipoandaa tulifanya pia *external review* kukaribisha taasisi za Kimataifa wakazipitia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie jambo moja, taasisi moja ya Uingereza ilipokuja hapa tulikaa nao, waliposoma Mpango wetu na dira yetu, wakasema: "Uchumi wenu umekuwa ukikua vizuri miaka yote 20. Hata mkibaki hivi hivi mlivyo, mkafanya mambo kama mnavyofanya bila kubadilisha chochote, uchumi wenu utaongezeka mara mbili na nusu mpaka mara tano."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mkibaki hivi hivi ifikapo mwaka 2050 uchumi wenu unakaribia kwenda Dola za Kimarekani bilioni 500. Wakatuambia, "kama mkibadilisha mwenendo, mkafanya mambo isivyo kawaida, badala ya kutembea, mkaanza kukimbia, *what they called business unusual* mnaweza uchumi wenu ukakua ukaenda zaidi ya shilingi trilioni moja ifikikapo mwaka 2050. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta binafsi walipokutana na wenyewe wakawa na maoni hayo hayo. Kwa hiyo,

tulipompelekea Rais mapendekezo, tulipeleka *scenario* zote hizi. Tulipomweleza Rais, kwa ujasiri mkubwa, aliamua, akachagua, na kuelekeza kwamba tuende na *business unusual,* kwenda kwenye shilingi trilioni moja, lakini *it is only possible if we begin doing things, business unusual*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa uniruhusu nieleze hapa kwa mujibu wa Mpango ambao tumeuwasilisha, mambo kumi ambayo lazima tuyafanye ili ku-*attain business unusual*. Jambo la kwanza, ni lazima tubadilishe mtazamo kuhusu kazi ya dola kutoka kuwa mdhibiti kwenda kuwa mwezeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni muhimu kabisa, na kwa kweli tunatafakari mapendekezo ya Kamati ya Bajeti, wamependekeza kwamba tuwe na *regulatory authority* moja, tuvunje zote zilizopo, tuwe na moja ili kuondoa kero. Hili ni pendekezo kubwa, tumelichukua, na Serikali italitafakari tuone namna ya kulitekeleza. Hoja ya msingi hapa ni kwamba, ni lazima Serikali ipunguze udhibiti iende kwenye uwezeshaji. *(Makofi)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Najma M. Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, muda wako umeisha naomba umalizie.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuanza kupimana kwa kuzingatia matokeo na viashiria vinavyopimika badala ya kupimana kwa kuangalia shughuli ambazo mtu amezifanya. Hapa tunapimana sana kwa shughuli. Mtu yupo *busy* anafanya shughuli nyingi kwa matokeo yapi? Kwa hiyo, Mpango unaeleza twende kwenye *results-based performance*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni kukubali kuchagua sekta chache ambazo ni *engine* ya ukuaji wa uchumi na kuzipa nguvu isiyo ya kawaida. Hapa Waheshimiwa Wabunge, turejee mchango makini sana wa Mheshimiwa Prof. Sospeter Mwijarabu Muhongo, wale wanaodharau elimu wasikilize mchango wa Mheshimiwa Prof. Muhongo kama ni wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumechagua sekta chache tisa za kimageuzi, na tumechagua vichocheo vitano ambavyo vitapewa msukumo usio wa kawaida ili uchumi wetu uweze kwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa ninamalizia. Jambo la nne ni kuifanya sekta binafsi kuwa sehemu muhimu kama nilivyosema awali. Hapa tukizungumzia sekta binafsi, hatuzungumzii malaika hapa. Sekta binafsi kama ilivyo sisi, watafanya makosa, lakini tuzingatie utawala wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la sekta binafsi, mtu mmoja anafanya makosa, anazomewa nchi nzima, haiwezi kutusaidia. Sekta binafsi moja ikifanya makosa, achukuliwe hatua za kisheria, kuliko kana kwamba sekta binafsi yote ni mbovu, hapana. Hii haiwezi kuwa sawa. Watakuwa na makosa, lakini tuzingatie utawala wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeainisha mambo mengine, lakini la mwisho niliseme, kujenga utamaduni wa kuheshimu utawala wa sheria. Hili ni muhimu kabisa, hatuwezi kufanya mipango hii bila kuzingatia utawala wa sheria. Haya ni mambo ambayo lazima tukubali, lakini kujenga utamaduni wa kukumbatia weledi, utaalam na wenye weledi na wataalam, uadilifu na waadilifu, uwajibikaji na wawajibikaji, na mwisho kuchapa kazi na wachapakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu tuna utamaduni kidogo. Mtu akichapa kazi sana, wakati mwingine wanasema huyu naye anajipendekeza, anataka uteuzi, ahaa, tuache hizo. Watu wanaochapa kazi, wenye weledi, wenye uadilifu, tuwaheshimu, tuwakumbatie, ni jambo la msingi sana hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, nihitimishe kwa kusema tu, hapa duniani tunayo mambo mengi ya kushukuru ambayo tumebarikiwa nayo, na wakati mwingine hatuwezi kuyamaliza yote kuyasema, lakini mambo matatu hatuwezi kuacha kuyashukuru. Kwanza, tunapaswa kushukuru kwa anayetupa uhai, neema, rehema na baraka. Huyu ni Mungu na Mungu pekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tunapaswa kumshukuru mtu anayetupa hifadhi na kututunza, hapa ni familia. Tatu, tunapswa kumshukuru mtu anayetupa fursa ya kutumikia umma kwa kuwa siYo kila mtu ana fursa hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii adimu na adhimu kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa fursa aliyonipa ya kutumikia katika Serikali yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa, kwa fursa aliyonipa ya kuongoza mchakato wa kuandika nyaraka ambazo zitaongoza mustakabali wa nchi yetu kwa miaka 25 ijayo, hili kwangu ni jambo kubwa, ni upendeleo wa kipekee na sitausahau katika maisha yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwamba wengi hapa wamenipongeza, lakini wasisahau, wamenipongeza, wameuona uwezo wangu kwa sababu nimepewa fursa. Kama nisingepewa fursa, wasingefahamu uwezo wangu. Ninamheshimu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu amenipa fursa hii, nao wakaniona. Ninamshukuru Mheshimiwa Samia, na Mungu ambariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mdogo wangu, Baba Levo amesema pale, ametoa historia yetu kidogo. Ni kweli, hapa duniani ipo hadithi moja. Alikuwa anakimbia ndege maarufu angani, ikatokea baridi na theluji, akazidiwa, akaanguka anasubiri kufa. Kwa bahati nzuri, akawa anapita pundamilia, akamnyea. Kile kinyesi kwa sababu kilikuwa ni cha moto, kinyesi kikawa pona yake, akapata joto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, duniani hapa siyo kila kinyesi ni kibaya. Mdogo wangu Baba Levo, siyo kila teke ni baya. Kuna teke ukipigwa linakupeleka pazuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie. Serikali imepokea maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge na tutayazingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo kwa kuwasilisha hoja hiyo ya kuhitimisha na kupokea maoni ya Waheshimiwa Wabunge kwa uzito unaostahiki, ahsante sana.

Sasa hivi ninamkaribisha Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Khamis Mussa Omar ili aweze kuja ku-*wind up*. Karibu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote na mimi ninaomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kufika asubuhi ya leo na kuweza kufikia majumuisho ya michango ya Waheshimiwa Wabunge katika Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo na Mwongozo wa Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninaomba nimshukuru Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa uongozi wenu katika mjadala wote huu tuliokuwa nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana ilikuwa tarehe 5 Februari, 2026. Miaka 49 iliyopita siku kama ya jana, katika Uwanja wa Amani Zanzibar vyama viwili vya ukombozi *TANU* na *ASP* viliunganishwa na kuzaliwa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie fursa hii kumpongeza sana Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Taifa kwa kuadhimisha miaka 49 ya Chama Cha Mapinduzi. Ni matumaini yangu kuwa chama hiki kitaendelea tena kuongoza katika miaka 49 ijayo na kitaendelea kuleta maendeleo makubwa kwa wananchi wa Taifa hili, ikizingatia yale ambayo wananchi wanayahitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliwasilisha Mapendekezo ya Mwongozo wa Bajeti, na tulipokea maoni na michango kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge, ambapo kimsingi mwongozo huo umepata maoni ya namna ya kuimarishwa kabla ya kuweza kutolewa kwenda kwa Maafisa Masuuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, waliendelea kutoa ushuhuda wa kazi kubwa ya maendeleo iliyofanywa nchini kote katika muda wa miaka minne iliyopita, ya kipindi cha kwanza cha Awamu ya Sita ya Serikali ya CCM inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hakika sehemu kubwa ya michango ya Waheshimiwa Wabunge ilikuwa ni maoni ambayo tumeyapokea kwa heshima kubwa. Ninaomba uniruhusu nitoe maelezo mafupi kwenye maoni, hasa kutokana na yale ambayo yametokana na Kamati yetu ya Bajeti, ambayo mimi ni Mjumbe, kupitia uongozi wa Mwenyekiti mahiri Mheshimiwa Mashimba Ndaki Mbunge wa Jimbo la Maswa Magharibi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maoni ya Kamati moja ya hoja ambayo ilitolewa ilikuwa ni kuitaka Serikali kuangalia upya suala la kutenga asilimia tano ya mapato ya mifuko kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za kuendeleza miundombinu kwenye maeneo maalum ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipendekeza kama Serikali kwamba katika mifuko mbalimbali asilimia tano itengwe kwa madhumuni haya, lakini maoni ya Kamati ikawa kwamba tuliangalie hili na ikiwezekana kuliacha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunadhani kwamba, tutoe maelezo ya ziada kwamba maelezo yetu yanaambatana na yanaendana na maoni ambayo yametolewa na Waheshimiwa Wabunge ya haja ya kufungua fursa zilizoko katika mikoa na maeneo ya kijiografia mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia mikoa ya Mara, Mbeya, Kigoma na kwingineko kwamba kuna fursa kubwa za kiuchumi zinahitaji kuendelezwa na zinahitaji kufunguliwa. Sasa katika hili pendekezo letu lilikuwa siyo kubadili mfumo uliopo wa matumizi ya fedha za mifuko isipokuwa ni kuendana na uamuzi wa Serikali wa kuweka maeneo maalum ya kiuchumi katika kila mkoa. Kwa hiyo, pendekezo ilikuwa ni kwamba pale ambapo Mfuko wa *TARURA* au *TANROADS*

utapeleka barabara katika mkoa, sehemu ya barabara ziwe zinapelekwa katika maeneo haya maeneo huru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, mifuko ya maji, *UCSAF,* na mifuko mingine yote nayo ielekeze sehemu ndogo ya asilimia tano tu ielekezwe katika miundombinu katika maeneo ya kiuchumi ili tuweze kuyafungua haya maeneo na tuweze kutumia vizuri fursa ambazo zipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili lilikuwa ni marekebisho, ambapo Kamati ya Bajeti ilipendekeza katika ile 10% ya awali kwa ajili ya makundi maalum, vijana, wanawake na watu wenye ulemavu, tulipendekeza kuongeza asilimia nyingine tano ambayo nayo ikaonekana kwamba kuna tofauti ya uwezo wa halmashauri zetu, na kwamba pendekezo hili lilenge kwenye halmashauri ambazo zina uwezo pekee na zile nyingine zisubiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa pendekezo la Kamati lilikuwa ni kwamba, kwenye mwongozo tufanye marekebisho ili tuweze kuchukua haya maoni ambayo yamejitokeza na mwongozo elekezi iwe halmashauri zenye uwezo peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea ushauri huu na tumekubaliana nao. Isipokuwa niongeze tu kwamba, tunapokwenda katika mwaka unaofuata wa fedha tumekubaliana na wenzetu wa Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kwamba tutafanya *study* maalum kuangalia uwezo wa halmashauri zote na kuangalia mfumo ambao utakuwa mzuri zaidi kwenye kupunguza tofauti ya uwezo wa kimapato baina ya halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutatazama *horizontal physical imbalance* ambayo tunajaribu kui-*address* kwa utaratibu maalum. Kwa hiyo, hili tutalifanyia utafiti wa ziada na tutalitolea mwongozo baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu lilikuwa ni kuisaidia sana Mamlaka ya Mapato *(TRA)* kuweza kuimarika na kukusanya mapato yetu zaidi, hasa katika upande wa mifumo ya TEHAMA. Katika hili niseme kwamba, Serikali imekuwa ikichukua jitihada

kubwa sana za kuimarisha *TRA*. Mwaka huu tukijaliwa *TRA* itatimiza miaka 30 tangu kuanza kwake rasmi shughuli zake. Ilianza mwaka 1996 na mwaka huu itakuwa imetimiza miaka 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi katika miaka 30 hiyo takribani yote nimekuwa mdau wa *TRA*. Ninaijua *TRA* ilipotoka, nilikuwa mfanyakazi kwa miaka 12, nilikuwa katika *senior managers* wa *TRA* kwa miaka tano na nusu, na nimehudumu katika bodi yao kwa takribani miaka 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaifahamu *TRA* tulioanza nayo, haikuwa na mfumo wowote wa mapato. Leo hii *TRA* ina mifumo takribani 21 ya TEHAMA. Upande wa *Customs* wana mfumo mkuu mmoja unaitwa *Tancis* ambao unaungana na mifumo miwili mingine ya taasisi tofauti wa *Electronic Single Window System* na *TANOGA* ambao unaungana na mamlaka zote za udhibiti kwenye utoaji wa mizigo bandarini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mapato ya ndani kuna mifumo tisa, halafu kuna mifumo mingine miwili kwa upande wa malipo, na kwa upande wa utawala kuna mifumo tisa. Kwa hiyo, kwa ujumla *TRA* ina mifumo 21. Tumelichukua pendekezo la kuimarisha zaidi mifumo ya TEHAMA, lakini hili nilitaka tuliseme na tuliwekee maelezo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja kuhusu kutumia kifungu cha 13 (a) cha Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ili kuzisaidia benki za uwekezaji kupata mikopo kutoka nje ya nchi. Kwenye hili niseme, tumelipokea vilevile, lakini tunaupokea ushauri huu wa Kamati kwa tahadhari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa hivi Tanzania ina benki 42 ambazo zimeshapewa leseni na Benki Kuu, ikiwemo benki moja ya maendeleo *TADB*, benki moja ya uwekezaji *TIB*, benki 35 za biashara, benki mbili za jamii, na benki tatu za sekta ndogo ya fedha *(microfinance banks)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ushauri wa kwamba tuziruhusu benki kwenda kukopa nje, niseme kwamba kwa upande wa *TADB* tayari sheria ilishafanyiwa marekebisho na

inaruhusu hili, lakini inategemea na uwezo wa benki yenyewe kwa kutizama mizania ya benki. Kwa hiyo, kwa upande wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo *TADB,* hii imeshasaidiwa na imeweza kufanikisha mkopo kutoka nje wa shilingi bilioni 562 ambao umetokana na Benki ya Maendeleo ya Afrika na Shirika la Maendeleo la Japan *(JAICA)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazungumzo yanaendelea kwenye upande wa Benki ya Uwekezaji ya Ulaya *(EIB)* na tunatarajia nako itafanikiwa. Benki ya *TIB* inahitaji kwanza kuimarisha mizania yake ili tuje kuepuka hili jukumu la mkopo kuja kuhamia upande wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo limezungumzwa sana na Waheshimiwa Wabumbe pamoja na Kamati lilikuwa ni upande wa deni la Serikali na haja ya kuendelea kulidhibiti na kutumia vigezo vingine. Tumepokea ushauri, lakini niseme, kama ambavyo tumezungumza kwenye upande wa kuimarisha mapato na deni la Serikali, tumeendelea kuliangalia kwa ukaribu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukifanya uchambuzi wa kuangalia uhimilivu wa deni lenyewe, na kwa bahati takribani miaka yote kila tunapofanya uchambuzi imebadilika kwamba ni deni himilivu. Hata hivyo, nilitaka niseme, wakati tunaangalia deni letu, ni muhimu sana kuliunganisha na uwekezaji mkubwa, hasa kwenye maeneo ya miundombinu ambao unaendelea nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetumia wapi deni letu katika miaka iliyopita? Tukikamilisha ujenzi wa kipande cha kwanza mpaka cha sita *(lot 1 to 6)* za *SGR* itakuwa tumejenga kilomita 2,102 za reli ya kisasa ya *SGR* hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya ujenzi wa *SGR* reli iliyokuwa inaongoza ilikuwa ni *TAZARA* ambayo urefu wake ni kilomita 1,860. Kwa hiyo, *SGR* ambayo inaunganisha kutoka Mashariki kwenda Magharibi itakuwa ni ndefu zaidi kuliko reli ya muda mrefu tuliyokuwa tunajivunia ya *TAZARA*. Jumla ya dola bilioni 10 zitahitajika. Hadi sasa hivi bilioni nane zimeshatumika kwa madhumuni hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejenga Bwawa la Mwalimu Nyerere ambalo limeongeza uwezo wetu wa nishati mpaka kufika Gigawati nne na limegharimu takribani shilingi trilioni 7.542.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa miradi iliyopo ni ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Msalato hapa Dodoma ambao utakuwa na uwezo wa kuhudumia abiria milioni 1.5 kwa mwaka, na ambao utaweza kuhimili ndege za aina hii zikiwemo ndege za aina ya *Boeing 737* na *767 Dreamliner* kwa mara ya kwanza zitaweza kutua Dodoma. Kwa hiyo, pamoja na kwamba tunahitaji kuendelea kuangalia deni letu, lakini tuangalie deni lenyewe linatumika kwa ufanisi kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambalo nataka nilitolee ufafanuzi, ni suala la misamaha ya kodi, ambalo Waheshimiwa Wabunge nalo wamelizungumza sana; na Kamati ilipendekeza tufanye tathmini ya misamaha yote ya kodi na kuiondoa ile ambayo haina tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini zimeendelea kufanyika na tathmini ya mwisho ambayo ilifanyika mwaka 2021/2022 hadi 2024/2025 ilitoa matokeo mazuri. Kwa upande wa uwekezaji wa kawaida, ilionesha kwamba, katika kipindi hicho jumla ya miradi 2,293 iliwekezwa nchini, iliidhinishwa nchini, ambapo misamaha ambayo ilitolewa ilikuwa ni shilingi trilioni 1.35. Miradi hii ilipelekea kupatikana kwa ajira 666,940.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwa upande wa miradi ya uwekezaji ya kimkakati, jumla ya miradi 36 iliwekezwa nchini katika kipindi hicho, ambapo misamaha ya kodi iliyotolewa ilikuwa ni shilingi milioni 144,806.78; lakini kodi ambazo zililipwa kutokana na miradi hiyo ilikuwa ni shilingi milioni 931,953.81.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa miradi mingine, picha ambayo ilijitokeza ni hii hii, ambapo miradi hii ilichangia ajira 27,820. Kwenye upande wa misamaha ya kodi, kama nilivyosema, tumepokea ushauri mzuri na tutaendelea kuifanyia kazi yale yasiyo na tija ili misamaha isiyo na tija tuiondoe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo Mheshimiwa Waziri wa Mipango amezungumza, nchi yetu iko katika hatua ya uwekezaji na tunakoendelea tunaamini kwamba sekta itaendelea kuhitajika na tutahitaji uwekezaji mkubwa. Kwa hiyo, hapa tutahitaji kuleta uwiano mzuri baina ya uwekezaji pamoja na vivutio ambavyo tunavitumia kwenye uvutiaji wa misamaha hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, kulikuwa na swali moja ambalo lilijitokeza kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge liliulizwa kwamba, ni kwa nini upande wa Zanzibar haikujitokeza kabisa katika Mwongozo wala katika Mpango wa Maendeleo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka niseme tu, kwa mujibu wa utaratibu kwa mujibu wa Katiba na Muungano wetu, masuala yote yasiyo ya Muungano yanayohusu upande wa Zanzibar haya yako moja kwa moja chini ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Pia mamlaka ya kutunga sheria ambayo inasimamia na kupitisha bajeti zake ni Baraza za Wawakilishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunathamini kazi kubwa ambayo imefanyika katika miaka yote, lakini hasa katika kipindi hiki. Kwa upande Zanzibar, miradi ya kimkakati ambayo ilitakiwa ionekane humu, haiwezi kuonekana kwa sababu ya kikatiba na itaonekana katika mapendekezo ambayo yataanzishwa na SMZ kwa upande wa Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa niseme kwamba Serikali imepokea maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge na tutayazingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Khamis Mussa Omar, Waziri wetu wa Fedha, kwa kuhitimisha hoja hii ya Mpango na kwa kupokea maoni yote ya Waheshimiwa Wabunge kwa uzito unaostahiki. Ninaamini Mpango unakwenda kuwa mzuri na Mwenyezi Mungu atajalia ukatekelezeke vizuri.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

*(Bunge Lilirejea)*

*Hapa Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, nimeona niseme kabisa, wakati jambo la Mipango bado liko moto moto, kwanza tunapongeza sana Mawaziri kwa kazi kubwa mliyofanya, na Serikali kwa ujumla kwa namna mlivyojipanga. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna jambo ambalo nimelipenda, hili la kusema Bunge lisijadili kero za matundu ya choo. Sidhani kama hata halmashauri kama ya Ilala inatakiwa ijadili kero za matundu ya vyoo. Ilala tunakusanya shilingi bilioni 140 kwa mwaka. Ninaomba sana, haya mambo yetu haya, ninatoa mfano mdogo, Mheshimiwa Waziri Mkuu wewe umetuongoza vizuri sana kwenye fedha. Kwenye eneo la *tourism* Tanzania tumepata bahati kubwa sana kuwa na *Pope Leo,* Kiongozi Mkuu wa Wakatoliki ambaye ameishi Tanzania. *(Makofi)*

*Pope Leo* amekaa Tanzania, maeneo ya Morogoro, Songea, Dar es Salaam, na Zanzibar. Hivi tukiweka *Religious Historic Sites* shida iko wapi? Wanakuja wageni; wageni wanaokuja sio Wakristo tu, watu wengine wanafikiri hivi vitu ni vya Wakristo. Wanakuja wageni kutazama *Pope Leo* Morogoro alikuwa anakaa nyumba gani? Kanisa alilokuwa anasali Songea, marafiki wa *Pope Leo*, wazee wale bado wapo, ambao wanamjua, wameishi naye. Inawezekana na gari aliyokuwa anaendesha ipo. Hayo ndiyo maeneo. *(Makofi)*

Leo *Egypt* wana watalii milioni 19, wanakwenda kutazama jengo la *Pharaoh*, na vitu vya *Pharaoh*, ilhali *Pharaoh* hakuwa Mkristo wala Muislamu.

*Historic Sites* za Kiislamu, Kilwa kuna Msikiti una miaka 700. Kanisa la Zanzibar lina zaidi ya miaka 200 na kitu. Hii Wizara lazima ichangamke. *(Makofi)*

Ninakwambia Mheshimiwa Waziri Mkuu, *if you walk this talk* tukatafuta *experts, professionals*, tutapata watalii wa *Religious Historic Sites* siyo chini ya milioni nne kwa mwaka. Zaidi ya milioni nne kwa mwaka watu watakuja. *(Makofi)*

Kuna Waislamu wakishatoka *Umrah* hawataki kurudi makwao. Wanaweza wakaja hapa Kilwa, Bagamoyo, Zanzibar. Hoja hii ililetwa zamani, wakasema mnaleta mambo ya udini mambo ya udini. Hakuna suala la dini kwenye fedha. *(Makofi)*

Hii Mipango ya Mheshimiwa Rais, inahitaji fedha. Hatuhitaji maneno wala nyimbo. *We need revenue and we need it yesterday*. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ninakuomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kaa na watu wako, kaa na bodi yako tujaribu kuondoa hizi *unnecessary frictions* ambazo tunazo. Kuna aina tatu za watu aliniambia Mheshimiwa Prof. Kabudi. Watu *Nostalgic* ambao bado wana fikra za kizamani na maono ya kizamani. Kila kitu aah, hii zamani hatukufanya. *It is not about* zamani, *it is now*. *(Makofi)*

Pia, kuna watu *realistic* na kizazi cha sasa ni *impatient*. Hawataki kusubiri maendeleo yao. Vijana hawataki kusubiri maendeleo yao kabisa, *they want to see things working now for them*. Hakuna Taifa la vijana la kesho, vijana ni leo na ni lazima tubadilike. Lazima tubadilike! *(Makofi)*

*Frictions* za uchumi zimeshaondolewa kwa asilimia kubwa sana na Mheshimiwa Rais. Miundombinu tunayo, ndege tunazo, mawasiliano tunayo, barabara tunazo, madaraja tunayo, *trains* tunazo, tunangoja nini kwenda mbele? *(Makofi)*

Kwa hiyo, Serikali tunawaomba sana, na kweli Wabunge hawa tutabanana kweli kweli humu ndani. Sheria zetu bado siyo *friendly* kwa wawekezaji, siyo rafiki kabisa. Yote tunalinda nchi. Mtu anashindwa kusoma andiko, kimbilio lake la kwanza, hii kuna

usalama hapa, hapa kuna hiki, kuna hiki? Sasa hivi jamani mambo ya usalama, *everybody knows everything what you do. (Makofi)*

Sasa hivi usalama muda gani unakwenda kumpiga mwenzio? *It is not about* watu kujua nini *intelligence*, *it is open to everyone*. Leo tunahangaika na minara? Minara yenyewe inafungwa wala hawafuati taratibu za kisheria. Mnara mmoja una *distance* maalum ili *signals* ziwe sahihi. Ukiweka mnara mbali, *signals* zinapotea. Ndiyo maana wanasema huku hakuna *signal;* siyo sababu. *Displacement* ya minara inafanywa nje ya utaratibu, na ukiweka mbali, una-*transmit radiation* ambayo inaweza ikawaumiza watu.

Kwa hiyo, minara ina kiwango chake cha kuweka. Kwa hiyo, wafanyabiashara ili wa-*save* fedha wanaweka minara mitatu katika maeneo ambayo inatakiwa minara iwe minne au sita. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ninakuomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, wewe unajua namna gani ya kutafuta fedha. *Religious Tourism*; Zanzibar kuna Kanisa pale linapendeza, watu wangapi wanakwenda? Israeli, *how much money* wanaingiza kwenye *tourism* ya dini? Sasa, sisi tuna bahati tofauti. *Pope Leo* kaishi Tanzania. Tuweke miundombinu tutafute mtu aitangaze biashara. *(Makofi)*

Siyo unamtafuta mtu hapa hapa, unamtoa mtu sijui unamleta Zungu au mtoto wa Zungu, hapana. *A professional branding* ya hii kitu. *(Makofi)*

Mimi ninakwambia Mheshimiwa Prof. Muhongo, Mheshimiwa Waziri Mkuu, na Mheshimiwa Lukuvi, mtaona fedha zitakavyoingia Tanzania. Kila mwaka tutaongeza watalii milioni nne. Nchi ya jirani hapa, *tourism* wanaingiza *24 trillion*, sisi *12 trillion (may be 11 – 12)*, *why*? Morocco wanaingiza watalii milioni 16, *Egypt* milioni 19. Ndege tunazo, *infrastructure* tunazo, siasa bora tunayo, wananchi tunao, amani tunayo. *(Makofi)*

Kamati ya Bajeti, Mwenyekiti ninafikiri uko hapa. Tutapambana mpaka hiki kitu kiende mbele. Serikali chukueni hii

hoja muifanyie kazi. Watu watapenda kuona *Pope Leo* kasali wapi? Alikuwa anakaa wapi Peramiho? Benchi gani alikuwa anakaa?

Pia watu watapenda kuona Mashehe waliojenga Misikiti ya Kilwa, watu watapenda kuona meli iliyogeuzwa kuwa jiwe na watu wa Kilwa. *People want to see these things*. Tunavyo vivutio kibao, lakini *we are just sitting and doing nothing*. *(Makofi)*

Tukileta mradi, *no one cares*, kwa sababu mtu ana mshahara, ana gari, ana nyumba, hajali wenzake wanapata nini? Waziri wa Fedha uko hapa, Waziri Mkuu uko hapa, wewe mtu uko *very bright, intelligent*, una mapenzi, una uwezo mkubwa sana. Nendeni mkakae, *digest these things and see how we start*. *We would have to start this, yesterday,* wala siyo leo. *(Makofi)*

Hivi wangapi hapa kwenye Bunge hili wanajua kuwa *Pope Leo* ameishi Tanzania? Mnajua? Ni wachache! Morogoro, Songea, Dar es Salaam, Zanzibar, ndiyo maeneo yake. Sisi Waislamu tuna sehemu pale Madina ambapo Mtume wetu *Mohammed (S.A.W.)* ndiyo ulikuwa Msikiti wake. Eneo hilo ukienda kusali tunaaminishwa kuna thawabu nyingi unazozipata, na kila mtu anagombania kwenda pale. Ibada, lakini wenzetu wanaingiza fedha. Eeh, inaingia fedha. *(Makofi)*

Kuna Msikiti Abu Dhabi umejengwa miaka 13, huu Msikiti unasaliwa siku moja tu Ijumaa. Siku za kawaida ni *tourist area*. Kuna Msikiti *Morocco* (sisemi watu waingie Misikitini), maana watu watatafsiri vibaya. Ninajua nikishasema hapa itakuja hivi, mtu atalaaniwa huyu, au nini, lakini kuna maeneo ya Kilwa, Bagamoyo, hata maeneo ya Kusini huku kwa Mheshimiwa Shahibu, yako maeneo *historic sites* za kidini. Tubadilishe aina gani za utalii nchini mwetu. *We have to move forward* na kutazama namna gani tutaweza kusaidia Taifa letu. *(Makofi)*

Ninaomba sana Serikali, *we have to remove this friction*. *Mentality* za kizamani tuachane nazo. *Mentality* ya roho mbaya tuachane nazo. *Mentality* ya fitina tuachane nazo. *Mentality* ya mtu akifuatilia kitu inaonekana huyu ana maslahi ya fedha

tuachane nazo. Serikalini mtu akifuatilia kitu anaandika barua. *(Makofi)*

Mimi nitakwambia Mheshimiwa Waziri Mkuu, tulipata kero ya kupitisha bomba la majitaka kutoka upande wa Ilala kuingia upande kuvuka Mwendokasi. Ilibidi lazima kibali cha mshauri kitolewe, *TANROADS* tumeandika barua, kibali hakikutoka; kila mtu anaogopa kulingana labda na *interest.* Ilichukua zaidi ya miezi minne, *but it took me one day,* kibali kimetoka saa saba za usiku. Saba za usiku! Kama mtu anasema nina *interest*, *I have interest*. *Interest* yangu *I want to see this country moving forward* chini ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Tuna *pending MOU* ya Balozi mmoja; 18, (nitakupa baadaye Mheshimiwa Waziri Mkuu) *including* michezo Mheshimiwa Makonda. Tumekosa viwanja vya Qatar sababu hatukusanyi *MOU* zetu na hawa watu. Tunakosa misaada ya *irrigation*, *MOU* hazijasainiwa. *(Makofi)*

Ninapokutana na Mabalozi *I did a lot of work for this country*. Lazima tufanye kazi pamoja, na ninategemea uongozi wako Mheshimiwa Waziri Mkuu. Haya mambo, wewe kiongozi wangu ninakuomba sana. *Let us work together.* Bunge hili litakusaidia. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hii *generation* ya sasa hivi ni *impatient*. Mimi nimepata bahati, nina umri mkubwa na nimepita kwenye makundi yote hayo, lakini mimi nina ujana zaidi ya vijana. *I have* ujana *right in my heart*. Sijabadilika mimi. Mmeniona nimebadilika? *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Hapana!

**SPIKA:** Ninayasema haya kama utani, lakini *we have to move forward*. Haiwezekani kwenye eneo letu mtu akusanye shilingi trilioni 24 utalii, sisi tunakusanya shilingi trilioni 11 au shilingi trilioni 12. *Why? (Makofi)*

Tunduma, nimezungumza na Kamishna wa *TRA, he is doing a very good job*, anazungumza na *counterpart* Zambia. Vilevile, kuna *Lobito corridor* inaanza karibuni, *with this* mafoleni haya ya

kodi, kwa nini kusiwe na *One Stop Inspection*? Kwa nini kontena likitoka Dar es Salaam linatiwa hofu tukiwa Tunduma? *Why* lifunguliwe tena? Linafunguliwa sababu watu sijui wana nini, sijui. *We don't have to do this! (Makofi)*

Leo Mheshimiwa Waziri Mkuu ninakwambia yale makontena usione kama hakuna foleni, magari yanafichwa kwenye ma-*ICD* wanaogopa hizi foleni. Ndiyo maana hiyo *Lobito Corridor* (Angola, Zambia, *DRC*) *once it is done* watatukimbia, na imeandikwa changamoto ni hizi hizi tu *taxes*, kodi hizi. Hakuna *One Stop Centre*. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ninasema tumsaidia Mheshimiwa Rais. Mawaziri muwe na *innovation*. Msisubiri tu mpewe maelekezo, na nyie mje na mbinu zenu. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE**

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 37 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, ninaomba kutoa taarifa kwamba shughuli zote zilizowekwa kwenye orodha ya shughuli za Mkutano wa Pili wa Bunge sasa zimekamilika.

**SPIKA:** Hoja ya kuahirisha Bunge, Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote na mimi niungane na wenzangu kumshukuru Mungu kwa kutujaalia afya njema hadi leo tunapohitimisha shughuli zote zilizopangwa katika Mkutano huu wa Pili wa Bunge la Kumi na Tatu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba pia kutumia Bunge lako Tukufu kuendelea kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake

mahiri na juhudi zake za kuwatumikia wananchi kwa mapenzi ya dhati na jitihada za dhati.

Mheshimiwa Spika, sote ni mashahidi na tunatambua kazi kubwa anayoifanya katika maendeleo ya Taifa letu. Uongozi wake unaendelea kuwa chachu ya matumaini na dira ya mwelekeo wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaungana na Waheshimiwa Wabunge wote kumtakia kila la heri Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na afya njema, hekima na nguvu zaidi katika kutekeleza majukumu yake makubwa ya kuliongoza Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie pia fursa hii kukupongeza wewe mwenyewe pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kazi kubwa na nzuri ya kuliongoza Bunge letu. Wakati wa kipindi chote cha Mkutano huu wa Pili tumeshuhudia mkiongoza mijadala yote kwa umahiri wa juu, na sina shaka Waheshimiwa Wabunge wenzangu mtakubaliana nami kuwa, mafanikio ya Mkutano huu yametokana na weledi mkubwa wa Mheshimiwa Spika na wasaidizi wake katika kusimamia shughuli za Bunge. Ninakupongeza sana wewe pamoja na wasaidizi wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru pia Waheshimiwa Wabunge kwa pongezi zenu kwa Serikali na kwa michango yenye dhamira ya dhati ya kuboresha mipango na kazi zilizokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika kipindi hiki cha miaka mitano. Mjadala huu umeendelea kuthibitisha uimara wa Bunge katika kutekeleza wajibu wake wa Kikatiba wa kuishauri na kuisimamia Serikali kikamilifu. Michango na maoni yenu katika Mkutano huu vimepokelewa na vitafanyiwa kazi kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, tangu alipoapishwa na kuingia madarakani, Mheshimiwa Rais amefanya teuzi ambazo zimelenga kuimarisha utendaji na utoaji wa huduma kwa wananchi. Ninatumia nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na watendaji wengine walioteuliwa kwenye nyadhifa mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninatumia fursa hii pia kuwapongeza Wenyeviti: Mheshimiwa Najma Giga, Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso kwa kuteuliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge. Vilevile, ninawapongeza kwa kazi kubwa ya kusaidia katika kutekeleza majukumu ya kuliongoza Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia kutumia fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa kuwa Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati za Bunge za Kudumu. Ninaendelea kuwahakikisha kuwa, Serikali itafanya kazi bega kwa bega na itawapa ushirikiano wote unaohitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa, ninaungana tena na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salamu za pole kwa Bunge lako Tukufu kutokana na vifo vya Wabunge wenzetu wawili, Mheshimiwa Jenista Mhagama ambaye alikuwa Mbunge wa Jimbo la Peramiho aliyeaga dunia tarehe 11 Disemba, 2025 Jijini Dodoma. Pia Mheshimiwa Halima Nassor, Mbunge wa Viti Maalumu aliyeaga dunia tarehe 18 Januari 2026, Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, wakati wote tunaendelea kuwakumbuka na kukumbuka michango yao katika maendeleo ya Taifa letu. Mwenyezi Mungu awape pumziko la amani.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kuwapa pole Watanzania wenzangu wote waliopoteza ndugu, jamaa na marafiki waliopata madhara mbalimbali kutokana na ajali za barabarani na matukio mengine. Ninaomba Mungu awape subira waliopoteza ndugu zao, majeruhi wapone haraka, na Marehemu wapumzike kwa amani.

Mheshimiwa Spika, Mkutano huu kimsingi ni wa kwanza kujadili taarifa mbalimbali za Serikali katika Bunge la Kumi na Tatu. Nimefurahishwa na namna ambavyo Waheshimiwa Wabunge wenzangu mlivyotoa michango na ushauri wenu kwenye shughuli hizi za Kibunge. Hongereni sana, mnaendelea kukidhi matarajio ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na shughuli nyingine za Bunge, Mkutano wa Pili wa Bunge la Kumi na Tatu ulipokea na kujadili taarifa ziuatazo: -

(i) Hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa wakati wa ufunguzi wa Bunge la 13;

(ii) Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu (2026/2027 – 2050/2051);

(iii) Mapendekezo ya Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano Mitano (2026/2027 – 2030/2031);

(iv) Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027;

(v) Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi wa Mpango na Bajeti ya Serikali wa Muda wa Kati (2026/2027 – 2028/2029);

(vi) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2026 *(The Written Laws [Miscellaneous Amendments] Bill, 2026);* na

Muswada wa Sheria ya Mikopo kwa dhamana za mali zinazohamishika wa Mwaka 2026.

Mheshimiwa Spika, Kupitia Mkutano huu Waheshimiwa Wabunge wameuliza maswali 146 ya msingi na mengine 482 ya nyongeza ambayo yalijibiwa na Serikali. Halikadhalika maswali saba ya papo kwa papo yaliulizwa kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kufuatilia kwa umakini mijadala ya Waheshimiwa Wabunge, ambapo hoja zilizotolewa zimeonesha wazi kuunga mkono jitihada kubwa za Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo Waheshimiwa wameendelea kutoa maelezo na matarajio yao ya kuona miradi hiyo, hususan maji, nishati, barabara na miundombinu mingine ikikamilika kwa haraka ili wananchi waweze kunufaika kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, tayari nimewaelekeza Waheshimiwa Mawaziri: Waziri wa Fedha, Waziri wa Ujenzi, Waziri wa Maji, Waziri wa Nishati pamoja na TAMISEMI, kuandaa mchanganuo wa kina wa miradi yote iliyoainishwa na inayoendelea kutekelezwa kwa kusuasua ama kusimama.

Mheshimiwa Spika, mchanganuo huo pia uhusishe miradi ambayo ilishasainiwa lakini haijaanza kutekelezwa ili ambayo hati zake zimewasilishwa na malipo hayajafanyika kuweka mkakati madhubuti wa kukamilisha malipo na hatimaye kuhakikisha utekelezaji wa miradi hiyo unaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninatoa maelekezo mahususi kwa Waheshimiwa Mawaziri husika kuhakikisha zoezi hili linakamilika kabla ya kuanza kwa vikao vya Bunge vya Bajeti ili hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wameziibua ziweze kuwa na majawabu na taarifa ya utekelezaji wa hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezitoa.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kuwa tarehe 2/2/2026 Waziri wa Mpango na Uwekezaji na Waziri wa Fedha, waliwasilisha Bungeni Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu 2026/2027 – 2050/2051 na mapendekezo ya Mpango wa Nne wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka mitano, yaani 2026/2027 – 2030/2031, Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Muda wa Kati yaani 2026/2027 – 2028/2029 na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Spika, Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu umeainisha malengo mahususi na afua kwa kuzingatia shabaha na vipaumbele vilivyoainishwa katika Dira ya 2050. Kwa kuzingatia ongezeko la watu nchini na athari zake katika upatikanaji wa ardhi, huduma za jamii, miundombinu, umuhimu wa kuharakisha mageuzi ya kiuchumi na kukuza

uwekezaji, Mpango Elekezi umeweka mkazo maalumu katika maeneo sita yafiatayo: -

(1) Upangaji miji endelevu na unaozingatia utunzaji wa mazingira;

(2) Ushirikishwaji mpana katika kupanga mipango ya maendeleo;

(3) Kuongeza wigo na ubora wa huduma za jamii;

(4) Kuongeza tija katika kilimo, uzalishaji viwandani na utoaji wa huduma kwa kuongeza kasi ya matumizi ya teknolojia ikiwemo matumizi ya digitali, ubunifu na uongezaji thamani wa mazao mbalimbali;

(5) Kuweka mazingira rafiki na yanayotabirika ya uwekezaji na kufanya biashara ili kuweza kuvutia mitaji kutoka sekta binafsi ya ndani na nje ya nchi; na

(6) Kufanya mageuzi katika mfumo wa utawala na mabadiliko ya utamaduni na mitazamo.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Nne wa Mendeleo wa Taifa wa Miaka mitano yaani 2026/2027 – 2030/2031 una dhima ya mageuzi kwa ajili ya ukuaji wa uchumi jumuishi na uzalishaji wa ajira. Hatua hii inaweka msukumo wa kipekee katika kutekeleza mageuzi makubwa yatakayobadilisha mifumo, mitazamo na mwenendo katika utendaji ili kuchochea tija katika uzalishaji na kuongeza uwezo wa nchi katika kushindana kikanda na Kimataifa na kuchochea muunganiko wa sekta mbalimbali. Lengo ni kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha usafiri na usafirishaji wa bidhaa, viwanda, biashara, katika kanda na Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/2027, nia ya kwanza katika utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano, maeneo ya kimkakati yaliyopendekezwa kupewa kipaumbele katika mpango huo ni kujenga uchumi imara, jumuishi

na shindani kwa kufanya mageuzi ya mifumo ya utendaji ya taasisi na kuimarisha utawala bora.

Mheshimiwa Spika, pili, kuimarisha uwezo wa watu na maendeleo ya kijamii ili kuwa na watu wenye ujuzi, afya na wanaoweza kuhimili mabadiliko; tatu, kuimarisha miundombinu ya kidigitali, nishati na usafirishaji fungamanishi; nne, kuimarisha sekta zinazochochea uzalishaji unaoongeza thamani na ukuaji jumuishi; na tano, kuimarisha uhifadhi wa mazingira na uwezo wa nchi katika kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mapendekezo ya mwongozo wa maandalizi wa Mpango na Bajeti ya Serikali katika muda wa kati, kati ya 2026/2027 na 2028/2029 Serikali itatekeleza vipaumbele katika miradi inayoendelea, iliyosainiwa pamoja na vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka mitano. Maeneo mahususi ya kipaumbele katika matumizi ni kugharamia miradi ya kielelezo, kimkakati na miradi inayoendelea.

Mheshimiwa Spika, tutabana matumizi katika maeneo yasiyo ya lazima, yasiyoathiri shughuli za Serikali ili fedha hizo ziweze kuelekezwa kwenye miradi ya maendeleo. Tutaelekeza fedha katika kulipa deni la Taifa, mishahara ya watumishi wa umma na huduma za jamii. Tuna mambo makubwa ambayo yapo mbele yetu likiwepo jambo la utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote, ambayo imeanza na makundi maalumu, lakini pia na mabadiliko ya mitaala ambayo itaanza kutekelezwa siku siyo nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2026/2027, maelekezo ya kimakakti kwa Maafisa Masuuli ambayo yanapaswa kuwa na msukumo wa pamoja: Moja, Serikali imepanga kuongeza asilimia tano kwenye mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu inayotokana na mapato ya ndani ya halmashauri.

Mheshimiwa Spika, ninaelekeza Ofisi za Wakuu wa Mikoa pamoja na Wakuu wa Wilaya kusimamia mamlaka za Serikali za Mitaa kutumia kwa pamoja asilimia tano kati ya zile 15% ambazo zinatolewa kwenye mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye

ulemavu kwa ajili ya uwekezaji kwenye miradi ya kuboresha mazingira ya kufanyia biashara, yaani miundombinu, ujasiriamali ili kuweza kuvutia kuongeza fursa za ajira kwa makundi haya.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kufafanua kwenye hoja za Wabunge, Mheshimiwa Mbunge aliongelea kuwa kwenye awamu ya tano yalifanyika maelekezo ya Wafanyabiashara wadogo wadogo kupewa vitambulisho, na kwamba sasa hoja hiyo imekufa, la hasha! Hoja hiyo haijafa bali imeboreshwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, awali, kitambulisho kilikuwa kinagharimu takribani shilingi 20,000 na hakikuwa cha kidigitali na kilikuwa kinatumika kwa mwaka mmoja tu. Kwa sasa kitambulisho kinachotolewa ni cha kidigitali na kinadumu kwa miaka mitatu. Kwa hiyo, inapoonekana kwamba, katika baadhi ya miaka haifanyiki fanyiki kwa baadhi ya watu ni kwa sababu kitambulisho wanachotumia sasa kinatumika kwa miaka mitatu na ni kitambulisho cha kidigitali.

Mheshimiwa Spika, maana yake nini? Ni kwamba kitambulisho hicho kimeunganishwa na mifumo mingine ikiwemo mfumo wa *NIDA*. Awali kitambulisho hicho kilikuwa hakijaunganishwa na mifumo mingine kwa sababu hakikuwa cha kidigitali. Kwa sasa kwa kutumia kitambulisho hicho, aliyepewa, mnufaika, anaweza kukitumia kama dhamana kuweza kupata mkopo kwa sababu kina taarifa zote zile ambazo zipo kwenye mfumo wa *NIDA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tangu kitambulisho hicho kibadilishwe na kuwa cha kidigitali, kilipoboreshwa tangu Januari, 2025 hadi sasa, mwaka mmoja umepita. Matokeo yake, zaidi ya shilingi bilioni 10.9 zimeshatolewa na wanufaika zaidi ya 5,347 wameshanufaika nacho. Kwa hiyo, zoezi hilo linaendelea na utekelezaji wake utaendelea kuboreshwa zaidi na zaidi ili wanufaika wengi zaidi waweze kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Maafisa Masuuli wanakumbushwa kuzingatia mkakati wa kulinda wawekezaji wa ndani kwa kutoa kipaumbele cha kwanza katika zabuni na masharti ya mikataba, na malipo ya hati za madai; na tatu, Maafisa Masuuli kuandaa

mikakati ya kuzalisha na kulea na kukuza wajasiriamali wadogo, wa kati, na wakubwa kupitia dhana ya ushirikishwaji wa wananchi katika utekelezaji, uwezeshaji na upatikanaji wa mikopo ya gharama nafuu ili kuwezesha uibuaji wa fursa za ajira, hususan kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, taasisi na mashirika ya umma, hususan yanayojiendesha kibiashara yaweke mikakati ya kuondokana na utegemezi wa ruzuku kutoka Serikalini ifikapo Juni, 2029 ili kutoa fursa kwa Serikali kutekeleza miradi ya maendeleo inayowahusu wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunazikumbusha pia mamlaka za Serikali za Mitaa kuongeza uwazi katika utekelezaji wa miradi katika halmashauri zetu. Mapato yote yajulikane kwa Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Madiwani. Masuala ya mapato na fedha za miradi ya maendeleo isiwe siri. Kila wakati Katibu Tawala wa Mikoa wanapopokea fedha na kuzisambaza kwenda kwenye halmashauri zetu, watoe nakala Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, Ofisi ya Mbunge, Meya, Wenyeviti wa halmashauri pamoja na Madiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimemwelekeza Mheshimiwa Waziri, aandike barua kwa Maafisa Masuuli wote kuweka uwazi huo. Waheshimiwa Wabunge, kila mradi unaotekelezwa mpate nakala, miradi ambayo ipo hatua za kutekelezwa, na kila fedha zinapokuja, fedha za miradi, Ofisi za Wabunge, Mameya, Wenyeviti wa halmashauri, Madiwani wapate nakala za fedha ambazo zimeshakuja na aina za miradi inayokwenda kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuongeza uwazi, pia nimeelekeza ratiba za vikao vya Baraza la Madiwani, zizingatie ratiba ya vikao vya Bunge. Vikao vya Bunge siyo vya dharura, hata leo tutakapoahirisha Bunge tutataja vikao vya kukutana tena. Kwa hiyo, ni rahisi kwa vikao vya halmashauri kupangwa kwa kuzingatia ratiba hizo za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na maana Wabunge kuwa Wajumbe wa Vikao vya Mabaraza ya Madiwani. Tusitumie

mazoea ya kuwatoa Wabunge kwenye vikao hivyo vya halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miradi yote ambayo ipo kwenye hatua za utekelezaji, gharama zake zijulikane na fedha zitakazokwenda kutekeleza miradi hiyo zijulikane. Lengo la kuweka uwazi huu ni kuweza kuwasaidia Wabunge pamoja na Wawakilishi wengine kuweza kufuatilia utekelezaji wake, thamani ya fedha na hali halisi ya utekelezaji wa miradi ili waweze kuishauri na kuisimamia Serikali vizuri.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha utekelezaji wa maelekezo haya, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge, mnaporejea majimboni fuatilieni kwa karibu utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika maeneo yenu na ninaelekeza, wekeni hata mawe ya msingi, na zindueni miradi katika maeneo ambayo iko tayari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile hakikisheni mnapata taarifa za utekelezaji wa kila mradi na maeneo ambayo mnashauri tutumie fursa zote zilizopo katika maeneo hayo, tumieni fursa za Vikao vya Halmashauri, tumieni fursa za Vikao vya Baraza la Ushauri la Wilaya *(DCC)*, tumieni Vikao vya Baraza la Ushauri la Mkoa *(RCC)*, Wizara za Kisekta na ikibidi hata Ofisi ya Waziri Mkuu, kama kuna jambo ambalo mnaona linahitaji lichukuliwe hatua.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mchango wa sekta binafsi, katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ni mkubwa, niungane na Waziri wa Mipango na Uwekezaji kutoa rai kwa viongozi na watendaji wote Serikalini kuhakikisha tunathamini na kuhakikisha sekta binafsi katika hatua mbalimbali za kupanga na kuwashirikisha sekta binafsi katika hatua mbalimbali za kupanga na kutekeleza miradi yote ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, sekta binafsi ipewe heshima kama ambavyo sekta ya umma inavyopewa ili kuweza kuhakikisha ule ubia wa sekta ya umma pamoja na sekta binafsi unaleta maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bunge lako limepata muda wa kuchangia na kushauri Serikali juu ya Mipango na Mwongozo wa Maandalizi wa Bajeti kama ilivyowasilishwa hapa Bungeni. Aidha, tunaliahidi Bunge lako Tukufu kuwa, tutafanyia kazi maoni na ushauri, vyote vilivyotolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, sote tunakumbuka kuwa wakati wa Kampeni za Uchaguzi wa Mwaka 2025, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alitoa ahadi mbalimbali kwa wananchi. Ahadi hizo zipo na zile zilizoahidiwa kutekelezwa ndani ya siku 100 baada ya Serikali kuingia madarakani.

Mheshimiwa Spika, ahadi za Mheshimiwa Rais, zimeendelea kutekelezwa kikamilifu na Waheshimiwa Mawaziri wa kisekta, wamekuwa wakitoa taarifa za utekelezaji na mafanikio yaliyopatikana. Nitumie fursa hii kwa muhtasari kuainisha baadhi ya mafanikio ambayo yameshapatikana katika utekelezaji wa ilani, na yale ambayo yameshapatikana katika utekelezaji wa ahadi za siku 100.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa afya, Serikali imepata mafanikio makubwa ikiwemo kuongeza wigo wa upatikanaji na ufanisi wa utoaji wa huduma za afya hapa nchini. Mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya afya ni pamoja na haya yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, kuendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Bima ya Afya kwa Wote kwa awamu ya majaribio ambao unahusisha makundi maalumu ya Watoto, wazee, wajawazito na watu wenye ulemavu; kugharamia kwa 100% matibabu ya vipimo vya kibingwa kwa magonjwa sugu yasiyoambukiza yakiwemo, saratani, figo, moyo, sukari, mifupa na mishipa ya fahamu.

Mheshimiwa Spika, pia kuondoa zuio la kuchukua miili ya Marehemu katika vituo vya umma vya kutolea huduma za afya kwa kigezo cha madeni kote nchini na kufanya uwekezaji mkubwa wa miundombinu ya afya; kuajiri watumishi wa afya 5,000 na kuwapangia vituo vya kazi kote nchini; kutoa zaidi ya

shilingi bilioni 39 ili kuboresha huduma za uzazi na watoto wa changa katika vituo 89 vya kutolea huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuongeza vituo vya upasuaji wa dharura kutoka vituo 523 kwa Oktoba, 2025 hadi vituo 578 Januari, 2026 na kuongeza uwezo wa Taifa kukabiriana na athari za VVU na UKIMWI kwa kuhakikisha utoshelevu wa dawa za kufubaza makali ya UKIMWI kwa kufufua Kiwanda cha *Tanzania Pharmaceutical Industries* kilichopo mkoani Arusha na kuongeza fedha za ndani kupitia Mfuko wa Udhamini wa Afua za UKIMWI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Elimu, Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa upatikanaji wa elimu bora katika ngazi mbalimbali, lengo ni kuwezesha wanafunzi wa Kitanzania, kupata ujuzi utakaomudu ushindani wa Kitaifa na Kimataifa. Hivyo, mafanikio yaliyopatikana ndani ya siku 100 ni pamoja na kuzindua Mpango Mkakati wa Kisayansi wa Kujenga Umahiri wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu unaolenga kuhakikisha watoto wa darasa la tatu anasoma na kuandika na kuhesabu bila shida.

Mheshimiwa Spika, pia kuajiri walimu na kuwapangia vituo vya kazi, walimu 7,000 kama ambavyo iliahidiwa wakati wa kampeni wakiwa ni walimu wa masomo ya Sayansi na Hisabati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kuimarisha Mpango wa Pamoja kati ya waajiri, vyuo vya ufundi stadi pamoja na vyuo vikuu kwa lengo la kufungamanisha, kulinganisha mafunzo na mahitaji ya sekta za kipaumbele; kuimarisha matumizi ya TEHAMA shuleni kwa kusambaza vifaa katika shule za msingi na sekondari; kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu kwa kuendelea kutoa mikopo ya elimu ya juu kupitia mikopo ya wanafunzi pamoja na ufadhili kutekeleza Mpango wa Elimu Bila Ada kwa shule za msingi na sekondani; na kuendeleza tafiti na ubunifu kupitia mfuko maalumu wa *Samia Commercialization Fund* ili kukabilisha ubunifu na teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maji, katika kuhakikisha upatikanaji wa maji ya uhakika kwa matumizi ya nyumbani, kilimo,

mifugo na shughuli nyingine za kiuchumi Serikali imetekeleza yafuatayo: -

(i) Serikali imeanza ujenzi wa Gridi ya Taifa ya Maji kwa kukamilisha usanifu na upembuzi yakinifu wa miradi mikubwa ya kimkakati ikiwemo ule wa kutoa maji Ziwa Victoria hadi Dodoma kupitia Singida pamoja na miradi ya kipaumbele ya maji ya Mto Rufiji katika Mkoa wa Dar es Salaam, Pwani pamoja na Lindi na Mto Ruvuma katika Halmashauri za Mtwara Mikindani; *(Makofi)*

(ii) Upande mwingine ni kuendelea maandalizi ya miradi ya kupeleka maji kutoka Ziwa Tanganyika kwenda Mikoa ya Kigoma, Katavi pamoja na Rukwa;

(iii) Kufanikisha kukamilika kwa miradi 16 ya maji na kuendelea na ujenzi wa miradi 71 mingine ya maji itakayowanufaisha Watanzania zaidi ya milioni tatu kote nchini; na

(iv) Kulipa fidia kwa wananchi na kusaini mikataba ya kuboresha huduma za majisafi na usafi wa mazingira katika mikoa ya Mbeya, Njombe, Geita, Singida, Mwanza pamoja na Morogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua dhamira na msisitizo wa Mheshimiwa Rais katika kuhakikisha upatikanaji wa maji kwa Watanzania, tarehe 2 Januari, 2026 nilifanya ziara ya kutembelea na kukagua maendeleo ya ujenzi wa Bwawa la Kidunda, ambapo nilijionea binafsi hatua iliyofikiwa ya utekelezaji ambayo ni zaidi ya 40%.

Mheshimiwa Spika, hakika, mradi huu ukikamilika utaendelea kutatua changamoto ya maji kwa mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Morogoro ikiwemo (Ngerengere na Gwata) pamoja na maeneo ya Mkoa wa Tanga (Kwasunga kule Handeni). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kazi kubwa ya Mheshimiwa Rais, ameruhusu kufanyika kwa mradi huo, nilielekeza

Wizara ya Fedha na Wizara ya Maji kuharakisha malipo ya hati zilizokuwa zimewasilishwa ya kiasi cha shilingi bilioni 24.83.

Mheshimiwa Spika, nimepewa taarifa kwamba kiasi hiki tayari kimeshalipwa hapo tarehe 31 Januari, 2026. Nielekeze Wizara ya Maji kuendelea kusimamia kwa ukaribu utekelezaji wa mradi huo ili ukamilike kwa wakati kama maelekezo yalivyotolewa na Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa nishati, Serikali imeendelea kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia na kupata mafanikio makubwa. Mafanikio haya yanaimarisha upatikanaji wa nishati ya uhakika kwa matumizi ya kijamii na kiuchumi na kuharakisha maendeleo ya Taifa. Sambamba na hilo, Serikali imefanikisha mambo yafuatayo:-

(i) Kuwezesha upatikanaji wa majiko banifu na mitungi ya gesi *(LPG)* kwa ruzuku; *(Makofi)*

(ii) Kuendelea kuhamasisha taasisi zinazolisha watu zaidi ya 100 kwa siku kuhamia katika matumizi ya nishati safi ya kupikia;

(iii) Ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia na kuanza kuunganisha katika nyumba kwenye Mikoa ya Lindi na Pwani;

(iv) Mafanikio mengine ni kuandaa mazingira ya uzalishaji wa nishati mbadala kupitia mitambo ya mkaa mbadala katika mikoa ya Tabora na Dodoma;

(v) Mafanikio mengine ni kutekeleza miradi ya kuunganisha umeme kwa wateja wapya;

(vi) Kukamilisha awamu ya kwanza ya mradi wa kuzalisha umeme wa jua wa *Megawatt* 50 wilayani Kishapu mkoani Shinyanga utakaounganishwa katika Gridi ya Taifa; na *(Makofi)*

(vii) Mafanikio mengine ni kuendelea kutekeleza miradi ya kupeleka umeme katika vitongoji 9,009 yenye thamani ya zaidi ya

shilingi trilioni 1.2 kama tulivyoshuhudia utiaji saini wake ukifanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uwezeshaji wananchi kiuchumi, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuwawezesha wananchi kiuchumi. Hatua ambazo zilizochukuliwa ni pamoja na: -

(i) Kuongeza upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya biashara ndogo ndogo, za kati, na kampuni changa. Mnamo tarehe 05 Februari, 2026 nilishiriki kwenye tukio muhimu la uzinduzi wa utoaji mitaji yenye thamani ya shilingi bilioni 200 ili kuwawezesha wakulima, wafugaji, wavuvi, wafanyabiashara, maafisa usafirishaji, wasanii na kampuni changa za vijana kuongeza mitaji, kukuza biashara na kuchangia ajira na ukuaji wa uchumi;

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa sifa alizonazo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan mojawapo ni anapoahidi anatekeleza, tayari shilingi bilioni 200 zimeshakutoka. *(Makofi)*

(ii) Pia, mafanikio mengine ni kutoa mikopo mingine yenye masharti nafuu kupitia mifuko mbalimbali na kunufaisha wafanyabiashara wadogo, wajasiriamali na kampuni changa; na

(iii) Kuwatambua na kuwasajili wafanyabiashara wadogo zaidi ya shilingi milioni 100 na kuwapatia mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 707.4 kutoka taasisi za fedha *(NMB, DCB* na *TCB*). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie Bunge lako Tukufu kutoa rai kwa Watanzania kuendelea kutumia taasisi za kifedha zilizo rasmi na kuepukana kwenda kwenye taasisi za uchochoroni ambazo zinatoa mikopo ya kausha damu. Hakuna benki yenye masharti mabaya kuliko yale ambayo baadhi yetu Watanzania tunaenda kuyapata kwenye kausha damu. Twende kwenye taasisi zetu rasmi, tusiziogope, tukapate utaratibu wa mikopo iliyo rasmi ili kujiepusha na matatizo ambayo yamekuwa yakijitokeza kwenye baadhi ya taasisi ambazo hazijasajiliwa na riba zake haziko *regulated* na zinaleta matatizo kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine yaliyopatikana kwenye sekta ya fedha, ni kuimarisha sekta ya fedha. Serikali imeendelea kuboresha usimamizi wa mapato na uthabiti wa uchumi. Maboresho hayo yamewezesha kuongezeka kwa makusanyo ya mapato ya ndani na kuvuka malengo yaliyowekwa.

Mheshimiwa Spika, hatua hiyo imewezesha Serikali kutekeleza ahadi mbalimbali zilizotolewa na Mheshimiwa Rais ikiwemo ya kugharimia huduma za jamii, miradi ya maendeleo na uwezeshaji wananchi kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, mathalani, katika kipindi cha Novemba hadi Desemba, 2025 Mamlaka ya Mapato Tanzania, imekusanya shilingi trilioni 6.99 sawa na 101.89% ya lengo la kukusanya shilingi trilioni 6.86. Hayo ni mafanikio makubwa na ndiyo yanawezesha miradi hii kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninazielekeza Wizara za Kisekta ambazo hazijakamilisha utekelezaji wa ahadi za Mheshimiwa Rais kwa kutoa taarifa kuhakikisha Mpango wa Utekelezaji wake unakamilika na taarifa hizo zinatolewa. Kukamilika kwa utekelezaji wa ahadi hizo iwe ni kigezo cha utendaji ndani ya Serikali. Pia, niendelee kuelekeza uimarisha wa utoaji wa huduma bora kwa wananchi kwa kujenga miundombinu na kutatua kero za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kilimo, Serikali kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini ilitoa utabiri wa mwelekeo wa msimu wa mvua za vuli kwa kipindi cha kuanzia Oktoba hadi Desemba, 2025 na mwelekeo wa mvua za msimu zilizoanza Novemba, 2025 hadi Aprili, 2026.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyotabiriwa, mvua za vuli zilikuwa chini ya wastani katika baadhi ya maeneo na hivyo kuathiri ukuaji wa mazao, pamoja na mavuno. Hata hivyo, kipindi cha nusu ya pili ya msimu wa mvua mwezi Februari, 2026 hadi Aprili, 2026 kinatarajiwa kuwa na ongezeko la mvua ikilinganishwa na nusu ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, hali ya mazao mashambani inaendelea vizuri na mazao mengi yapo katika hatua za ukuaji. Katika maeneo yanayopata mvua za vuli baadhi ya mazao yameanza kuvunwa hususan mahindi na maharage. Kadhalika, mazao mengine yapo katika hatua mbalimbali za ukuaji na yanaendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwaelekeza Maafisa Ugani kuendelea kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wakulima kwa wakati. Aidha, niwakumbushe wakulima kuhakikisha wanazalisha mazao yanayokomaa kwa muda mfupi hasa katika maeneo yale ambayo yalitolewa utabiri kwamba huenda yasiwe na mtiririko wa mvua za kutosheleza.

Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa chakula nchini ni ya kuridhisha. Hii imetokana na uzalishaji wa mazao ya chakula katika msimu wa kilimo 2024/2025 kuwa mzuri ambapo uzalishaji ulifikia tani milioni 23.8 ikilinganishwa na mahitaji ya tani milioni 18.3. Uzalishaji huo umeihakikishia nchi utoshelevu wa chakula kwa 130%.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hiyo nzuri ya upatikanaji wa chakula hapa nchini, bado kuna maeneo ambayo uzalishaji wake haukuwa wa kuridhisha. Hivyo, Serikali inaendelea na tathmini ya kina kubaini hali ya chakula katika maeneo hayo na kuchukua hatua stahiki. Niwatoe hofu wananchi wote wa Tanzania, hapatakuwepo na mwananchi ambaye atapoteza maisha kutokana na kukosa chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, akiba ya chakula ya Taifa imeendelea kuimarika ambapo hadi kufikia mwezi Desemba, 2025, kiasi cha akiba ya chakula kilichohifadhiwa na Wakala wa Hifadhi ya Taifa ya Chakula kimefikia tani 578,072. Kuimarika kwa usalama wa chakula nchini kumetokana na uzalishaji mzuri wa mazao ya chakula ukiunganishwa na jitihada mbalimbali za Serikali ambazo imefanya ikiwemo utoaji wa ruzuku za pembejeo za kilimo, kuimarishwa kwa miundombinu ya umwagiliaji, huduma za ugani, zana bora za kilimo na upatikanaji wa mbegu bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jitihada hizo zinatokana na maono na dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuendeleza kilimo na kuwasaidia wakulima hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada hizo, hivi karibuni ameridhia utekelezaji wa mkakati wa Taifa wa Zana za Kilimo unaolenga kuimarisha matumizi, uzalishaji, usimamizi na uratibu wa teknolojia za kilimo katika mnyororo mzima wa thamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kupitia mkakati huo, Serikali imepanga kununua matrekta 10,000 na kuanzisha vituo jumuishi 1,000 vya huduma za zana za kilimo katika ngazi ya kata. Hivyo, utekelezaji wa mkakati huo utaleta mageuzi makubwa katika sekta ya kilimo na kuwanufaisha wakulima wengi huku Serikali ikishirikiana na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, hakika, Mheshimiwa Rais anastahili pongezi kwenye hili, kwa kuitoa sekta ya kilimo kutoka kwenye kilimo cha kauli mbiu kwenda kwenye uhalisia wa utekelezaji wa programu za kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie Bunge lako Tukufu, kuielekeza Wizara ya Kilimo kuendelea kusimamia kikamilifu sekta ya kilimo ikiwemo miradi ya umwagiliaji, kuongeza thamani ya mazao na uhifadhi wa mazao.

Mheshimiwa Spika, niwakumbushe Maafisa Ugani na Maafisa Kilimo kutoa elimu kwa wakulima kuhusu kanuni bora za kilimo na matumizi ya teknolojia za uhifadhi wa mazao. Kwa upande mwingine, nitoe wito kwa wakulima kutumia vizuri mavuno wanayopata sambamba na kuzingatia maelekezo ya wataalamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na uandikishaji wanafunzi wa darasa la awali, darasa la kwanza na wanafunzi wanaosoma kupitia Mpango wa Elimu Msingi Kwa Waliokosa (MEMKWA). Hadi tarehe 23 Januari, 2026, idadi ya wanafunzi wa darasa la awali walioandikishwa ni 1,049,015 (wavulana wakiwa

522,267 na wasichana wakiwa 526,748) wakiwemo wenye mahitaji maalumu 1,316 (wavulana 716 na wasichana 600). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hao, idadi ya wanafunzi wa darasa la kwanza walioandikishwa ni 1,341,112, wakiwemo wavulana 665,936 na wasichana 675,176; wakiwemo wenye mahitaji maalum 2,080; wavulana 1,137 na wasichana 943.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa elimu ya sekondari, idadi ya wanafunzi wa kidato cha kwanza walioripoti hadi kufikia 23 Januari, 2026 ni wanafunzi 510,474; wavulana wakiwa 234,389 na wasichana 276,085. Wakiwemo wenye mahitaji maalumu 1,116, wavulana wakiwa 571 na wasichana 532. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, idadi ya wanafunzi walioripoti kidato cha kwanza hadi sasa bado hairidhishi. Ninatoa maelekezo kwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kuhakikisha watoto wote waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza wanaripoti shuleni. Vilevile, nitoe wito kwa wazazi na walezi wenye watoto walio na sifa ya kuandikishwa darasa la awali au la kwanza, wahakikishe wanatekeleza wajibu huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ufaulu wa wanafunzi wa Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne umekuwa ukiongezeka ambapo kwa mwaka 2025 jumla ya watahiniwa wa shule 526,620 kati ya 555,606 sawa na 94.98% walifaulu Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne ikilinganishwa na mwaka 2024 ambapo watahiniwa 440,847 kati ya 477,262 walifaulu sawa na 92.37%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matokeo haya yametokana na Serikali kuendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika shule zetu ikiwemo kununua na kusambaza vitabu milioni 18 vya ziada.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii mbele ya Bunge lako Tukufu kuweka msisitizo kuhusu maeneo muhimu ninapoelekea kuhitimisha hotuba kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa utekelezaji wa miradi kwa ubia, Serikali haiwezi kuwa mtekelezaji pekee wa miradi yote ya maendeleo na kwa wakati mmoja kwa kutegemea rasilimali za Serikali peke yake. Sekta binafsi ni mdau mkubwa katika maendeleo na injini ya kuchachusha utekelezaji wa miradi mbalimbali. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali imeweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kutekeleza miradi ya maendeleo kwa ubia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, ninaielekeza Wizara ya Fedha kupitia Kituo cha Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Ubia kuhakikisha kinaratibu sekta zote na kutoa ridhaa kwa miradi yote nayokidhi vigezo ya kuendeshwa kwa ubia. Ninaomba nirudie tena hiyo, ninaielekeza Wizara ya Fedha kupitia Kituo cha Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa kutumia ubia kuhakikisha kinaratibu sekta zote na kutoa ridhaa kwa miradi yote inayokidhi vigezo ya kuendeshwa kwa njia ya ubia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Maafisa Masuuli wote wahakikishe wanatoa kipaumbele na ushirikiano kwa sekta binafsi zenye uwezo na kutekeleza miradi ya maendeleo kwa ubia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunakokwenda tutaanza kupima utekelezaji wa miradi iliyotekelezwa kwa bajeti ya Serikali na kupima miradi ile ambayo ilikuwa na sifa za kutekelezwa kwa ubia, tuone utekelezaji wake na tupime na kujiridhisha juu ya utekelezaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapoelekea kumaliza, pia niendelee kusisitiza haya yote tunayoyapanga ili yaweze kutekelezwa ni lazima tuzingatie amani, usalama na utulivu katika nchi yetu. Amani, usalama na utulivu ni jukumu la kila Mtanzania na linahitaji juhudi za pamoja katika nyanja mbalimbali. Hivyo tunawajibika kuepuka masuala yote yanayochochea uvunjifu wa amani ndani ya nchi yetu ikiwemo matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii. Pamoja na jukumu hili, ninapenda kukumbusha Watanzania wote masuala yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Wizara za kisekta, Wizara zenye dhamana ya ustawi wa jamii ziweke kipaumbele

kwa kushirikiana wadau mbalimbali wakiwemo viongozi wa dini na asasi za kiraia na mashirika yasiyo ya Kiserikali kutoa elimu na malezi yakiwemo matumizi bora ya mitandao ya jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawaasa Watanzania wenzangu kuwa na matumizi chanya ya mitandao ya kijamii na kuifanya kuwa nyenzo muhimu ya kujielimisha, kuendeleza biashara zetu na kukuza uchumi badala ya kuitumia katika njia ambayo inatugawa na njia ambayo inaleta athari hasi kwenye ukuaji na ustawi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe rai kwa Watanzania wote kulinda tunu hii ya amani kwa ajili ya Taifa letu na kwa kuwa ni wajibu wa kila raia, kuziheshimu na kuendeleza mshikamano na kudumisha amani katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sote tunatambua Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, alishatoa uelekeo na amekuwa mstari wa mbele katika kuleta mshikamano na maridhiano ndani ya nchi yetu. Hii inajidhihirisha kupitia maamuzi yake ya kuunda Tume Huru ya Uchunguzi wa Matukio ya Uvunjifu wa Amani yaliyojitokeza baada ya uchaguzi. Mapendekezo hayo ya Tume hiyo yataweka msingi kuelekea uundwaji wa Tume ya Mazungumzo na Maridhiano kama alivyoahidi kuiunda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali sikivu ya Awamu ya Sita itaendelea kusikiliza ushauri na maoni ya Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote, ili kuweza kuhakikisha tunakuwa na Taifa moja lenye watu wanaoheshimiana, watu wenye amani na furaha ndani ya nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, itakumbukwa kuwa, siku ya Jumatatu, tarehe 3 Novemba, 2025, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aliapishwa rasmi kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ishara ya utekelezaji na Ilani ya Uchaguzi imeanza kutekelezwa. Hiyo ndiyo ilikuwa ishara ya kwanza ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi kwa Mwaka 2025 - 2030. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawahakikishia Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwamba Serikali itatekeleza kikamilifu ilani kwa kuzingatia vipaumbele ambavyo vimeainishwa kwenye kila ibara kwa lengo la kuhakikisha kauli mbiu ya "Kazi na Utu, Tunasonga Mbele" inatekelezwa. Hivyo, nawakumbusha viongozi wa Wizara na Idara zilizo chini ya Idara zote za Serikali kuzingatia masuala muhimu ambayo yameainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi, nawasisitiza viongozi wote kuendelea kuwasikiliza wananchi. Waheshimiwa Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Watumishi wengine wote wa umma watenge muda wa kusikiliza wananchi na kutatua kero zao.

Mheshimiwa Spika, wananchi katika maeneo mbalimbali wanahitaji kuona kero zao zinatatuliwa. Nawaelekeza viongozi wote tutembelee maeneo ya wananchi, hususan yenye migogoro na tuyatafutie ufumbuzi. Ipo migogoro kwenye maeneo ya ardhi pamoja na maeneo mengine, wafuateni wananchi, wasikilizeni na tatueni kero zao, ili wasilazimike kwenda ngazi za juu au kusubiri ziara za viongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa michezo, nchi yetu imeendelea kufanya vizuri katika michezo mbalimbali. Mafanikio hayo yanatokana na maono na uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambapo katika uongozi wake tumeshuhudia mageuzi makubwa katika sekta ya michezo hapa nchini. Kutokana na hatua hizo, timu zetu za ngazi mbalimbali zimeendelea kufanya vizuri na kulitangaza Taifa letu Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii adhimu kuwapongeza vijana wetu wa Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu, *Taifa Stars,* kwa kufanikiwa kuandika historia ya kufuzu hatua ya 16 Bora ya Michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika. Tangu kuanzishwa mashindano haya, Tanzania imefanikiwa kushiriki mara nne; mwaka 1980 nchini Nigeria, mwaka 2019 nchini Misri, mwaka 2023 nchini Côte d'Ivoire na mwaka 2025 nchini Morocco, ambapo tumeweka rekodi ya kuingia hatua ya 16 bora. Mashindano ya *AFCON* hutazamwa na watu wengi duniani, hivyo, mafanikio

haya yameiwezesha Tanzania kutambulika zaidi katika ramani ya soka Barani Afrika na duniani kote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania, Baraza la Michezo la Taifa, Benchi la Ufundi, Wachezaji pamoja na wadau wote wa michezo imeelekeza nguvu katika maandalizi ya Timu ya Taifa, ili kuhakikisha inafanya vizuri zaidi katika mashindano yajayo ya *AFCON* 2027, ambayo yatafanyika kwa umoja nchini Tanzania, Kenya pamoja na Uganda. Aidha, maandalizi ya miundombinu mbalimbali, ikiwemo ujenzi na ukarabati wa viwanja, yanaendelea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matarajio yetu ni kuhakikisha maandalizi yanafanyika kwa ufanisi na kombe hilo linabaki hapa nchini na inawezekana. Natoa wito kwa Watanzania wote kuendelea kuiunga mkono timu yetu ya Taifa wakati wote na kuchangamkia fursa mbalimbali zinakatojitokeza kutokana na maandalizi ya mashindano hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, ninatumia fursa hii, Timu zetu za Taifa za michezo mingine zimeendelea kufanya vizuri katika maeneo mbalimbali. Mathalani, katika mchezo wa kriketi, Timu ya Taifa ya Vijana Chini ya Umri wa Miaka 19 ilifanikiwa kufuzu Mashindano ya Kombe la Dunia la Kriketi Chini ya Umri wa Miaka 19 yaliyofanyika mwezi Januari, 2026 nchini Namibia. Hatua muhimu katika maendeleo ya michezo ni pamoja na hiyo.

Mheshimiwa Spika, timu nyingine zilizofanya vizuri katika hatua mbalimbali za mashindano ni pamoja na Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu ya Wanawake "*Twiga Stars*", Klabu ya *JKT Queens,* Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu Chini ya Umri wa Miaka 20, yaani *Ngorongoro Heroes*. Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu kwa Watu Wenye Ulemavu, yaani *Tembo Warriors,* Timu ya Taifa ya Ngumi, Timu ya Taifa ya Kuogelea na Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu Chini ya Umri wa Miaka 17, yaani *Serengeti Boys*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia kuzipongeza klabu zetu za soka hapa nchini kwa mafanikio makubwa zinazoendelea

kuyapata katika mashindano ya Kimataifa. Klabu za Michezo za Simba na Yanga; Aah, nianze na Yanga na Simba. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Timu ya Yanga na Simba zimeonesha ushindani wa hali ya juu kwa kufanikiwa kufuzu na kushiriki katika hatua za Makundi ya Ligi ya Mabingwa Barani Afrika. Hali hii inadhihirisha uimara, ubora na ukuaji wa soka la Tanzania katika ngazi ya Afrika. Kwa kuwa, michezo bado inaendelea, ninazitakia kila la heri katika michezo inayofuata.

Mheshimiwa Spika, aidha, Klabu za Azam na *Singida BS* zimefanikiwa kufuzu kushiriki hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Barani Afrika. Mafanikio haya yameendelea kuitangaza vyema nchi yetu na kuipa heshima kubwa Kimataifa, pamoja na kuongeza alama za nafasi ya Tanzania katika viwango vya soka hapa Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, kuendelea kukuza vipaji vya michezo, hususan miongoni mwa vijana wetu, Serikali inaendelea kutekeleza kwa kasi na ujenzi wa Akademia ya Michezo ya Malya. Mradi huu ni moja ya uwekezaji mkubwa wa kimkakati unaolenga kuandaa kizazi kipya cha wanamichezo mahiri watakaoweza kushindana katika ngazi mbalimbali za Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii kuipongeza Klabu ya Yanga kwa kufanikiwa kutwaa ubingwa wa Kombe la Mapinduzi katika fainali iliyochezwa katika Uwanja wa Gombani, Pemba, dhidi ya Klabu ya Azam. Mashindano ya Kombe la Mapinduzi siyo tu ni burudani, bali yamekuwa chachu ya mshikamano wa Kitaifa, unaoenzi Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar na kukuza vipaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua na kuthamini mchango wa wanamichezo binafsi katika kulitangaza Taifa. Ninapenda kumpongeza Mwanariadha wetu mashuhuri Alphonce Simbu, kwa kuwa Bingwa wa Dunia wa Marathon katika mashindano ya riadha yaliyofanyika Jijini Tokyo, nchini Japan, ambapo alinyakua medali ya dhahabu. Mafanikio hayo

yameitangaza Tanzania Kimataifa na kulipa heshima Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nahitimisha hotuba yangu kwa kuwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu muhimu mliyoitoa kwa lengo la kuboresha maisha ya wananchi wetu. Kama nilivyotangulia kusema, michango yenu ni muhimu sana katika kuimarisha utendaji wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umesema hapa tutabanana, na sisi huku Serikalini tutabanana hivyo hivyo kwa sababu, Mheshimiwa Rais ameshaelekeza. Kama ambavyo umetoka kumsikia Waziri wa Mipango akisema, kwamba Mheshimiwa Rais amechagua, tutafanya kazi kwa hali isiyo ya kawaida, *business unusual*. Tutafanya kazi kwa kasi kubwa zaidi na hiyo ndiyo kauli aliyoitumia wakati analizundua Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninatoa rai kwa Watumishi wa Umma kila mmoja kwenye *desk* lake kuzingatia hiyo kauli ya *business unusual*. Tutaendelea kufuatilia utekelezaji wa kauli hiyo na maelekezo hayo ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Katibu wa Bunge, wasaidizi wake na watumishi wote wa Bunge kwa kutuhudumia vizuri na msaada mkubwa ambao wametoa katika kipindi chote wakiwa hapa. Kadhalika ninawashukuru viongozi wa vyombo vya ulinzi na usalama kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kulihakikishia usalama Taifa letu, Waheshimiwa Wabunge na wageni wetu na hatimaye leo tunahitimisha Mkutano huu wa Kumi na Tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninatoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu pamoja na Watumishi wote Serikalini. Mmefanya kazi kubwa na nzuri, na mmekuwa mkitoa ufafanuzi unaohusu sekta zetu kwa wakati na kwa weledi. Utendaji wenu umekuwa chachu ya mafanikio ya hii mijadala ambayo imefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, ninamshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kazi kubwa anayoifanya ya kutoa ushauri na ufafanuzi wa masuala yote yanayohusu sheria. Ninawashukuru

viongozi na watendaji wote Serikalini na taasisi zote ambao wameendelea kutekeleza majukumu yao kwa weledi, umahiri na ufanisi mkubwa. Hongereni sana kwa juhudi kubwa ambazo mnazifanya.

Mheshimiwa Spika, nimeendelea kusema kila wakati, Watendaji wa Serikali na Watumishi wa Umma ambao wanafanya kazi nzuri wasishikwe na unyonge wowote pale wanapokuta kuna walio wazembe wanachukuliwa hatua. Hatua ni kwa ajili ya wale wasiofanya vizuri, na pongezi ni kwa ajili ya wao wanaofanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, nchi hii inapiga hatua kwa sababu, wapo watumishi wanaofanya vizuri. Wapo Watumishi wa Umma wanaofanya vizuri, tena walio wengi wanafanya vizuri. Hongereni sana kwa kazi nzuri mnayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nitakuwa mchoyo wa fadhila endapo sitowashukuru wanahabari kwa uchambuzi mzuri walioutoa. Pia, ninawashukuru madereva wetu na niwatakie safari njema tutakapokuwa tunatawanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katikati ya mwezi huu Februari tunatarajia kuwa na ibada ya mfungo. Natumia fursa hii kuwatakia waumini wote wa Kiislamu maandalizi mema ya Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani na Waumini wa Kikristo maandalizi mema ya Mwezi Mtukufu wa Kwaresma. Kwa kuwa, hizo zote ni ibada muhimu kwa waumini wa madhehebu hayo ya dini, natoa rai kwa wafanyabiashara kutopandisha bei kwa kutumia kipindi hicho muhimu cha ibada.

Mheshimiwa Spika, hatuna uhaba wa chakula, hivyo tusipandishe bei, hatuna sababu ya kufanya hivyo. Tuache watu wafanye ibada kwa amani. Tuendelee kuiombea nchi yetu katika kipindi hicho cha ibada za Mwezi Mtukufu pamoja na Kwaresma. Tuendelee kumwombea Rais wetu pamoja na sisi sote. Natoa rai kwa Watanzania wote, tuendelee kudumisha amani na utulivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa ninapenda kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu liahirishwe hadi Jumanne, tarehe 31 Machi, 2026, saa 3.00 asubuhi, litakapokutana tena katika ukumbi huu hapa Jijini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia au kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge wote kuwa, kutakuwa na Uchaguzi wa Viongozi wa Bunge *Sports Club* utakaofanyika leo, tarehe 6 Februari, katika Ukumbi wa Msekwa mara baada ya kuahirisha Mkutano wa Bunge.

Uchaguzi huo utahusisha viongozi wafuatao: Mwenyekiti wa *Bunge Sports*, Makamu Mwenyekiti, Meneja, Wajumbe watano wa Kamati ya Utendaji *Bunge Sports,* angalau wanawake wawe wawili. Waheshimiwa Wabunge wote naomba mshiriki.

Mheshimiwa Zainab Katimba, Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Vijana Tanzania *(TYPC),* anaomba kuwatangazia Wabunge wote Vijana wenye umri chini ya miaka 40 kujisajili katika karatasi zinazopitishwa ukumbini hii leo, kama sehemu ya maandalizi ya kupata mawasiliano ya Wajumbe watakaounda umoja huo katika Bunge hili la Kumi na Tatu. Hivyo, wanaohusika mnaombwa kufanikisha zoezi hili kwa kujaza majina kamili na namna ya mawasiliano ya *WhatsApp*. Fomu ziko hapa, ninamkabidhi Katibu.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI**

**WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI**

*(Hapa Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki Ziliimbwa)*

**SPIKA:** Endeleeni kusimama. Sasa nitawahoji kuhusu hoja ya Bunge kuahirishwa mpaka tarehe 31 Machi, 2026.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Ninaahirisha Shughuli za Bunge mpaka tarehe 31 Machi, 2026 saa 3.00 asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 6.57 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 31 Machi, 2026 Saa Tatu Asubuhi)*